# MATOKEO YA MATUMIZI YA UREJELEZI KATIKA MAHUSIANO KATI YA JAMII YA ABAGUSII NA KIPSIGIS

**NYAIGOTI PATRICK KEFA**

**Tasnifuhii imewasilishwakatika Halmashauri ya Masomo ya Shahada za Juu Kwa Madhumuni ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili, Chuo Kikuu cha Egerton**

**CHUO KIKUU CHA EGERTON**

**OCTOBA, 2024**

## UNGAMO NA IDHINI

**Ungamo**

Tasnifuhiini kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa na yeyote katika Chuo Kikuu chochote kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada yoyote.

Sahihi..... Tarehe.7/10/2024.

**Kefa P. Nyaigoti AM12/2466/0**

**Idhini**

Tasnifu hii imewasilishwa na kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Egerton

Sahihi. Tarehe 7th /10 /2024

**Prof. Catherine Kitetu**

Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu

Chuo Kikuu Cha Egerton

Sahihi. Tarehe7 October 2024

Idara ya Idara ya Lugha, Isimu na FasihiChuo Kikuu cha Pwani

Dr. Abdulrahim Hussein TaibAli

Idara ya Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi.

Chuo Kikuu cha Pwani

**HATILINZI**

© 2024, Kefa Patrick Nyaigoti.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kamwe kuiga, kunakili, kutafsiri au kuhifadhi tasnifu hii kwa njia yoyotebila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Egerton.

## TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwawazazi wangu kwa kunipa shime ya kiusomi ambayo iliniwezesha kufika hapa nilipo katika bahari ya kiakademia. Pia, naitabaruku kwa mke wangu, Isabella na wanangu Jannet, Geofrey, Elaine na Kennedy. Kazi hii iwe nguzo kwenu katika bahari ya kiusomi, muitunze vilivyo. Kwa wanafunzi wenzangu, asanteni kwa kunipa ushindani na motisha ya kuimaliza kazi hii. Kwa ndugu zangu wapendwa, Marehemu Kennedy Mong'are Nyaigoti na Daniel Osebe Nyaigoti, mlinipa ushindani na motisha katika bahari ya kiakademia ambayo ilinipa shinikizo ya kiusomi na kuimaliza kazi hii. Mungu aweke roho zenu mahali pema peponi.

**SHUKRANI**

Namshukuru mwenyezi Mungu kwa kunijalia na kunipa nguvu wakati wote wa uandishi wa kazi hii ya uzamili wangu na kuniwezesha kuikamilisha kazi hii. Kuhitimisha tasnifu hii ilitokana na watu kadhaa ambao ninawapa shukrani zangu za dhati. Nawashukuruwasimamizi wangu Prof. Catherine Kitetu na Dkt. Abdulrahim Hussein Taib Ali ambao walinipa motisha na shime ya usomi, kunielekeza na kuniongoza katika bahari ya uzamili. Walisoma kazi yangu pasi na kuchoka na kunipa mapendekezo ambayo yalinijenga kiusomi. Bila mwongozo wao, tasnifu hii haingefikia ufanisi huu. Asanteni sana wahadhiri wangu kwani tangu mwanzo mmekuwa waelekezi wangu kiakademia. Maelekezo na ushauri mlionipa ni dira maishani mwangu daima.

Namshukuru Prof. Hadija Murenga aliyekuwa mkuu wa Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii kwa imani yake kwangu. Dkt Raphael Gacheiya na Dkt Melvin Ouma ambao kwa makini walifuatilia hatua zangu kiusomi na kiutafiti ili kunisaidia kuhitimisha kazi hii. Shukrani zangu pia zimfikie aliyekuwa mwenyekiti wa Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu Dkt. D. Kweya, mwenyekiti wa sasa Dkt. Walunywa pamoja na wahadhiri wote idarani. Nawaombea baraka zake Maulana. Vilevile nawashukuru wazazi wangu na familia yangu kwa kunipa motisha ya kuikamilisha kazi hii.

# IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza matokeo ya matumizi yaurejelezi katika mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis. Jamii hizi zimekuwa na matumizi ya urejelezi ambayo wanaisimu hawajaifanya tafiti na kuitathmini. Utafiti huu uliongozwa na madhumuni yafuatayo: Kubainisha na kueleza lugha urejelezi inayotumiwa na jamii ya Abagusii na Kipsigis;Kujadili lugha rejelezi inayotumiwa na jamii ya Abagusii na Kipsigis na athari zake katika mahusiano yao na kutathmini mbinu za suluhu zinazotumiwa na Abagusii na Kipsigis kuunda uhusiano bora kati yao. Utafiti huu uliongozwa nandharia ya Utambulisho wa Lugha za Kikabila inayohusu makabila/mbariza binadamu na mahusiano kati ya jamii, yaani (‘Ethnolinguistics identity Theory’ (ELIT). Utafiti huu ni wa kithamano mkabala wa mfano (case study) na ulifanyika katika maeneo ya Borabu na Sotik ambapo ni mpaka ya jamii hizi mbili. Sampuli lengwa ilikuwa ya kimakusudi na ilihusu wazee wanaume 10 na kina mama 10 wenye umri wa miaka 60 na zaidi, kutoka jamii ya Abagusii na Kipsigis na vijana 20 wenye miaka 24 hadi 35 kutoka pande zote za Abagusii na Kipsigis wanaoishi eneo la Borabu – Sotik, kata ya Gelegele tarafa ya Ndanai na kata ya Esise tarafa ya Borabu, eneo hili ni mpaka wa jamii ya Abagusii na Kipsigis. Kwa jumla watafitiwa 60, watfitiwa 30 kutoka jamii ya Abagusii na watafiwa 30 kutoka jamii ya Kipsigis. Mtafiti alishiriki katika mazungumzo katika ukusanyaji wa deta na kisha kufanya unukuzi wa yaliyojiri. Deta ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo.Mtafiti alingundua kwamba lugha ya urejelezi huzua rabsha, vurugu na vita. Hivyo basi, wanaobuni sera hawana budi kushirikisha lugha ya urejelezi katika uundaji wa sera zao kuhusu matumizi ya lugha rejelezi ili kusuluhisha mitafaruku inayotokana na jamii zinazopakana. Utafiti huu utafaidi katika kuleta suluhu, amani na utengamano miongoni mwa jamii mbalimbali ulimwenguni, Afrika na Kenya. Utafiti huu utaelimisha jamii, hasa, asasi za serikali na wasimamizi wa kaunti, halmashauri ya kutatua ugonvi miongoni mwa jamii kitaifa, pamoja na kutoa kumbukumbu ambazo serikali kuu na kaunti zinaweza kutumia ili kuleta suluhu miongoni mwa jamii wakati wa mitafaruku. Aidha, matokeo yametoa kumbukumbu za marejeleo ambazo wasomi watatumia ili kufanya tafiti nyingine kati ya jamii mbalimbali kwani matumizi ya urejelezi huzua mitafaruku, rabsha na vita miongoni mwa jamii.

## ABSTRACT

This study investigated the outcome of the use of referential language used by Abagusii to refer to the Kipsigis and the referential language used by the Kipsigis to refer to Abagusii. The study investigated the implication of referential language on the relationship of the two ethnic groups and the effect of using referential language. The study was guided by the following objectives: To identify and explain the referential language used by Abagusii and Kipsigis to refer one another; to explore the implication of referential language used by Abagusii and Kipsigis to refer to each other and to evaluate how an agreeable relationship between Abagusii and Kipsigis is created as a result of use of referential language. The study was guided by Ethno linguistic identity theory (ELIT). This was a qualitative study, which used a case study perspective. The study was carried out in Sotik- Borabu, the boundary of the two counties and was confined further to Gelegele Location of Ndanai division and Esise Location of Borabu division. The target population for the study was10 old men and 10 old women aged 60 years and above from both Abagusii and Kipsigs community and 20 youths aged 24 years to 35years from Abagusii and Kipsigis communities living around the border, in total a sample size of 60 people, 30 from Abagusii and 30 from Kipsigis community. Data was analyzed and presented by description whereby the sampled community gave references they use to refer to each other. The use of referential language causes conflict and war between neighboring communities and therefore there is need to develop a policy to curb this vice. This study generate knowledge that will contribute to Education sector, discourse analysis in general that are useful to county commissioners who are administrators in the County and the National Council for Conflict Resolution.

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI........................................................................................II**

**HATILINZI ........................................................................................................III**

**TABARUKU.......................................................................................................IV**

**SHUKRANI .........................................................................................................V**

**IKISIRI ...............................................................................................................VI**

**ABSTRACT.......................................................................................................VII**

**ORODHA YA JEDWALI ....................................................................................XI**

**SURA YA KWANZA ..............................................................................................1**

**UTANGULIZI.......................................................................................................1**

1.1 Usuli wa mada.......................................................................................................1

1.2 Suala la utafiti ......................................................................................................3

1.3 Madhumuni ya utafiti............................................................................................4

1.4 Maswali ya utafiti .................................................................................................4

1.5 Umuhimuwa utafiti ..............................................................................................4

1.6 Upeo na mipaka ya utafiti .....................................................................................5

1.7Ufafanuzi wa Istilahi...............................................................................................6

**SURA YA PILI.......................................................................................................7**

**MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA...........................................7**

2.1 Utangulizi...............................................................................................................7

2.2 Mapitio ya Maandishikuhusu Urejelezi miongoni mwa Jamii mbalimbali .........................7

2.3 Misingi ya Nadharia..............................................................................................14

**SURA YA TATU..................................................................................................16**

**MBINU ZA UTAFITI...........................................................................................16**

3.1 Utangulizi.............................................................................................................16

3.2 Muundo wa Utafiti ...............................................................................................16

3.3 Mahali pa Utafiti ..................................................................................................16

3.4 Umma lengwa .......................................................................................................17

3. 5 Uteuzi wa Sampuli...............................................................................................17

3.6  Ukusanyaji wa Deta .............................................................................................18

3.7 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Deta ..................................................................19

3.8 Maadili ya utafiti....................................................................................................20
**SURA YA NNE ..........................................................................................................21**
**UCHANGANUZI, UWASILISHAJI NA UFASIRI WA DETA ......................................21**
4.1 Utangulizi.........................................................................................................21
4.2 Lugha ya Urejelezi Miongoni mwa Abagusii na Kipsigis.................................................21
4.2.1 Lugha Urejelezi wakati wa Uhasama kati ya Abagusii na Kipsigis ...............................23
4.2.2 Lugha ya Urejelezi Wakatiwa furaha ..........................................................................31
4.2.3 Lugha ya Urejelezi Wakati wa Ndoa...........................................................................34
4.3 Athari za Lugha ya Urejelezi katika Mahusiano ya Jamii ya Abagusii na Kipsigis..........37
4.3.1 Athari Hasi za Lugha ya Urejeleziambapo kuna dhana ya ‘sisi; na ‘wao’ .....................37
4.3.2 Athari Chanya za Lugha ya Urejelezi..........................................................................45
4.4. Mbinu za Suluhisho Zinazotumiwa na Abagusii na Kipsigis Kuimarisha Uhusiano Mwema kati yao..........................................................................................................47
4.5 Hitimisho............................................................................................................52
**SURA YA TANO .........................................................................................................53**
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .......................................................53**
5.1 Utangulizi.........................................................................................................53
5.2 Muhtasari .........................................................................................................53
5.3 Hitimisho............................................................................................................53
5.3.1Lugha ya Urejelezi miongoni mwa Abagusii na Kipsigis ...............................................53
5.3.2 Athari za Lugha ya Urejelezi katika Mahusiano ya Jamii ya Abagusii na Kipsigis.......56
5.3.3Mbinu za Suluhisho Zinazotumiwa na Abagusii na Kipsigis Kuimarisha Uhusiano......59
5.3.4 Mafanikio ya utafiti....................................................................................................60
5.3.5 Matatizo ya utafiti.....................................................................................................61
5.3.6 Mapendekezo ..........................................................................................................61
**MAREJELEO .............................................................................................................63**
Kiambatisho 1: Kanuni Za Unukuzi Wa Deta .......................................................................71
Kiambatisho 2: Kielelezo Cha Mahojiano.............................................................................71
Kiambatisho 3: Kielezo Cha Mahojiano Katika Vikundi Viini..............................................72
Kiambatisho 4: Fomu ya kukubali kushiriki katika utafiti- Jamii Ya Kipsgis ........................72
Kiambatisho 5: Fomu Ya Kukubali Kushiriki-Jamii Ya Abagusii.........................................73

Kiambatisho 6: Idhini Kutoka Chuo Kikuu Cha Egerton........................................................74
Kiambatisho 7: Idhini Kutoka NAKOST ....................................................................75
Kiambatisho 8: Ikisiri ya Makala Iliyochapishwa .....................................................76
Kiambatisho 9: Ramani inayoonyesha makaazi ya Abagusii -.................................77
Kiambatisho 10: Deta Ya Maingiliano Yasiyo Rasmi..............................................78

## ORODHA YA JEDWALI

Jedwali 1: Ratiba ya Ukusanyaji wa Deta....................................................................67
Jedwali 2: Udhanifu Wa Urejerezi kati ya Jamii ya Abagusii na Kipsigis..............................69

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa mada

Utafiti huu ulichunguza matokeo ya matumizi ya lugha rejelezi katika mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis.Lugharejelezi hutumiwa na jamii mbalimbali uliwenguni, barani Afrika na Kenya, kwa jumla. Matumizi ya urejelezi huuinakisiwa kuwa huenda ikawa ndio kiini cha kutoelewana, vurugu, rabsha na vita miongoni mwa jamii. Rabsha hizi zinatokana na tofauti za kidini kulingana na Elchinova (2001), kikabila, kulingana na Kang (2004). Zienkowski (2011), Drew (1998) na Guillem (2017) ambao walitafiti suala hili kwa muktadha wa misingi ya rangi. Ni kutokana na hali hii ambapo mtafiti alilenga kutafiti urejelezi kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis ilikubaini iwapo matumizi ya urejelezi huzua mitafaruku, kutoelewana na rabsha kati yao. Utafiti huu haujawai tafitiwa popote pale. Urejelezi huu una dhana hasi na chanya dhana chanya hukuza umoja na husiano mwema kati ya jamii ambapo matokeo yake ni suluhisho hasa kunapotokeavurugu, rabsha na mitafaruku inayohusishwa na matumizi ya urejelezi (Ajayi & Buhari, 2014).

Jamii ya Abagusii ambao vilevile wanajulikana kama Kisii ama Omogusiini mojawapo ya jamii za kundi la Bantu. Ni majirani wa jamii kama vile Kipsigis, Maasai na Luo (Hellen, 2016). Abagusii walitoka Misri kabla ya kuingia nchini Kenya kutoka Uganda kupitia Mlima Elgon. Wanapatikana Magharibi ya Kenya katika maeneo ya Kisii na Nyamira, katika eneo la Nyanza. Wanapatikana takriban kilomita hamsini mashariki mwa ziwa Victoria. Maeneo yao yana idadi kubwa ya watu na mashamba yao yana rotuba kubwa sana. Abagusii wamegawanywa katika vikundi saba vya kijamii ambavyo ni Abagitutu, Abagirango wa kaskazini na Abagirango wa kusini, Abamachoge, Abanjari (Nchari), Ababasi na Abanyaribari. Kama jamii zote za Kibantu, Hellen (2016) anadokeza kwambakitegauchumi cha jamii ya Abagusii ni ukulima. Mimea inayokuzwa katika maeneo haya ni kama vile; majani chai, kahawa, mahindi, mtama, mawele, muhogo na mboga. Jamii hii inajulikana sana kwa upanzi wa ndizi. Mbali na ukulima Abagusii wana mifugoingawa ufugaji wa mifugo ulianza baadaye sana katika maisha yao. Miongoni mwa Wabantu, Abagusii ni jamii inayoishi katika eno la kipekeekijiografia kwa kuwa wanazungukwa kutoka pande zote na jamii za Nailoti kama vile

Luo, Kipsigis, na Maasai (Odongo, 2009). Kwa misingi hii, Abagusii kinyume na jamii nyingine za Kibantu waliweza kujipata katika hali ya vita mara kwa mara hasa kwa sababu ya wizi wa mifugo na matukio ya kisiasa na jamii hizi za Nailoti na hivyo wakalazimika kujenga himaya yenye nguvu sana.

Kipsigis ni Wanailoti, wanaopatikana katika maeneo ya Bonde la ufa. Mahususi, wanaishi katika nyanda za juu ya maeneo ya bonde la ufa. Wanapatikana katika lugha mame ya Nilo-Saharan. Wanaishi katika maeneo ya Kericho na Bomet. Majirani ambao wamepakana na jamii ya Kipsigis ni pamoja na Abagusii, Luo na Maasai (Nyagosia, 2017). Kipsigis ni mojawapo ya lahaja ya Kalenjin. Kalenjin ni lugha iliyo na lahaja kama vile: Kipsigis, Nandi, Tugen, Marakwet, Pokot, Ndorobo, Keiyo na Terik. Wanapakana na jamii ya Abagusii maeneo ya Kaskazini na Kaskazini mashariki (Mwanzi & Henry, 1973). Kitega uchumi cha jamii hii ilikuwa ni ufugaji lakinikwa sasa wanafanya ukulimawa majani chai, mahindi, viazi vitamu na mtama miongoni mwa mimea mingine.

Mpaka kuu kati ya jamii hizi ni Mto Gucha (Kuja) ambao maji yake yanatumiwa na jamii hizi mbili. Jamii hizi pia hukutana sokoni na kutekeleza biashara zao kila juma, aidha wana ushirikiano wa karibu kupitia biashara ya ubadilishanaji na ndoa za mseto kati yao. Hali hii hukuza uhusiano mwema kati ya jamii hizi.

Urejelezi *Kamama, Bomori, batiab naAhure* ni urejeleziKipsigis hutumia kurejelea Abagusii kutokana nandoa baina yao. Kwa upande mwingine Abagusii wana urejelezi kama vile *Omonyamato, Matomasungunanu Omosani, Korera Omwabo* ambaoni urejelezi unaotumiwa na jamii ya Abagusii kurejelea jamii ya Kipsigis. Istilahi hizi zinaonyesha hali ya ushirikiano na amani kati ya jamii hizi. Hata hivyo kutokana na imani kuwa Abagusii ni Bantu na hivyo ni wakulima wala si wafugaji, kumekuwa na mitafaruku na vita kati ya jamii hizi mbili kutokana na wizi wa mifugo (Hellen, 2016). Ni kutokana na hali hii ambapo urejelezi chanya na hasi hutumika.

Jamii ya Kipsigis wanaamini kuwa wao ndio wafugaji wa wanyama (Monti na wenzake, 2023) na hivyo mara nyingi wanawashambulia Abagusii kwa lengo la kuiba mifugo yao hasa ng'ombe. Wakati huu ndipo urejelezi hutumika kwa hiyo ni bayana kusema kuwaurejelezi umechangia pakubwa katika vurugu, rabsha na uhasama kati ya jamii hizi mbili. Mbali na suala

la mifugo, matumizi ya urejelezi, uchaguzi mkuu wa nchi huzua ghasia kati ya jamii hizi mbili. Shughuli za siasa na uchumi ndio vianzo vikuu vya vurugu, rabsha na kutoelewana kati ya jamii hizi mbili za Abagusii na Kipsigis. Ingawa siasa ni mojawapo ya vianzo vya madhila haya, inabainika kuwa hali hii kati ya jamii hizi ilianza kitambo kidogo hata kabla ya 'joto' la siasa kushika kasi nchini Kenya. Hali hii hushika kasi Kenya inapoelekea kushiriki katika uchaguzi mkuu.

Lugha ina nafasi muhimu katika maisha ya mwanadamu. Lugha humwezesha mtu kutambua na kuamua iwapo anayekutana naye ni rafiki au adui (Wright, 1997). Anaongezea kuwa lugha hutumiwa kuonyesha umoja na kujenga uhusiano. Jabbar na Hassan (2018) wanaonyesha nguzo muhimu za lugha na wanasema kuwa lugha hutumiwa kama ufunguo wa utangamanowowote ule na vilevile hutumiwa kuonyesha umoja na kujenga uhusiano na utangamano. Wanasema kuwa nguzomuhimu katika mawasiliano na matumizi ya lugha yanajikita katika nguzo za unominishaji, urejelezi, udunishaji, uwakilishaji nauhusishaji. Urejelezihukuza uhasama ambao huzua vurugu, rabsha, mitafaruku na vita. Vilevile hukuza urafiki, ujirani mwema na hitimaye ndoa za mseto ambazo huleta jamii pamoja na kuleta suluhisho vita na uhasama vinapotokea kati ya jamii.

Urejelezi ni kifaa mojawapo kinachoweza kutumiwa kupima urafiki na au uadui. Rabsha na ghasia kati ya jamii hizi mbili huweza kugunduliwa kupitia hali hii. Wazungumzaji wanaweza kurejeleana kwa njia mbalimbali hivyo kufanya ule urejelezi kuchukuliwa kama mawasiliano ya kiurafiki au uchokozi. Urejelezi huwa unaambatanishwa na mawazo ganda. Matumizi ya urejelezi nchini Kenya hutumiwa na jamii mbalimbali maishani mwao (McOnyango, 1995). Hali hii huenda ndio hali sawia na uhusiano wa Abagusii na Kipsigis. Kwa hivyo, Utafiti huu ulichunguza matokeo ya matumizi ya lugha rejelezi katika mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis ambayo yamekuwa yakidhihirisha kutoelewana, rabsha na vurugu kati yao kwa muda mrefu.

### 1.2 Suala la utafiti

Dhima ya urejelezi ni: kujieleza, kujenga urafiki, kujenga uhusiano na ni kifunguo cha utangamano wa aina yoyote ile (Jabbar & Hassan, 2018). Wanadokeza kwamba watumizi wa lugha wanaweza kutumia lugha kurejeleana kutegemea kiwango cha utangamano kati yao.Hata

hivyo, ile hali ya urejeleziusipopolewavizuri na watumizi lugha, urejelezi huweza kusababisha kukosekana kwa maelewano na hatimaye kuzua mgogoro, rabsha na vurugu kati ya watumizi wa urejelezi. Utafiti huu ulichunguza matokeo ya matumizi ya urejelezi katika mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis.

### 1.3Madhumuni ya utafiti

i. Kubainisha na kueleza lugha rejelezi inayotumiwa na jamii ya Abagusii na Kipsigis.
ii. Kujadili lugharejelezi unayotumiwa na jamii ya Abagusii na Kipsigis na athari zake katika mahusiano yao.
iii. Kutathmini mbinuza suluhisho zinazotumiwa na Abagusii na Kipsigiskuimarisha uhusiano bora kati yao.

### 1.4 Maswali ya utafiti

Maswali yafuatayo yataongoza utafiti huu:

i. Jamii ya Abagusii na Kipsigis hutumia lugha gani ya urejelezi kurejeleana?
ii. Je, lugha ya urejelezi wanayotumia Abagusii na Kipsigis ina athari gani kwa mahusiano yao?
iii. Jamii za Abagusii na Kipsigis wana mapendekezo yoyote ya suluhisho kwa mitafaruku inayotokana na matumizi ya lugha urejelezi?

### 1.5Umuhimuwa utafiti

Utafiti huu ulichunguza urejelezi na vipengele vya kijamii na kitamaduni jinsi vinavyoathiri matumizi ya urejelezi miongoni mwa jamii za Abagusii na Kipsigis na kuelewa chanzo cha kutoelewana, vurugu na rabsha kati yao. Hii itatoa mchango katika taaluma ya Isimujamii ambayo hudhamiria kuelewa jinsi vipengele vya kijamii na kitamaduni huathiri matumizi ya urejelezi miongoni mwa jamii.

Vilevile utafiti huuutadokeza kwamba urejelezi miongoni mwa jamii ni jambo la kawaida kwani hii ni mojawapo ya tanzu ambazo zimekuwemo tangu jadi na zimekuwa zikitumika miongoni mwa jamii mbalimbali ulimwenguni, ila mara nyingi huchukuliwa kuwa matumizi yake yana nia mbaya dhidi ya jamii nyingine na kuzua rabsha, vurugu na vita.

Utafitihuuvilevileutaonyesha jinsi jamii itaishi kwa umoja na utangamano na jinsi ambavyo jamii itasuluhisha tofauti zao.

Utafiti huu utapanua mawanda ya marejeleo katika taaluma nyinginezo kama vile taaluma ya Isimu Jamiipamoja na kumbukumbu ambazo serikali inaweza kutumia ilikuleta suluhu kati ya jamii wakati wa mitafaruku kati yao. Pamoja na kuchangia katika kubainisha matumizi ya lugha katika muktadha mahususi. Kupitia kazi hii kutakuwa na msingi wa kulinganisha matumizi ya urejelezi katika muktadha mahususi. Hii sio tu nchini Kenya, bali kote ulimwenguni, kwani iwapo patakuwa na amani kupitia matumizi ya kumbukumbu hizi kati ya jamii moja na nyingine kuna uwezekano wa kupata suluhu na hivyo kusuluhisha vurugu, rabsha na kutoelewana miongoni mwa jamii. Matokeo ya utafiti huu yataweka wazi sifa za urejelezi miongoni mwa jamii hizi.

**1.6 Upeo na mipaka ya utafiti**

Walioshirikishwa katika utafiti huu walikuwa jamii ya Abagusii na Kipsigis.Katika utafiti huu sampuli ilihusisha wanaume wazee 10 na kina mama 10 kutoka pande zote mbili za jamii za Abagusii na Kipsigis, hawa walikuwa umri wa miaka 60 na zaidi. Aidha, vijana10kutokaupande wa jamii ya Abagusii na Kipsigis hasa waendeshaji wa bodabaoda walio naumri kati ya miaka 24 hadi 35. Kwa ujumla, watafitiwa 30 kutoka jamii ya Abagusii na 30 kutoka jamii ya Kipsigis walishiriki katika utafiti. Utafiti huu ulijikita katika mpaka wa jamii hizi mbili. Watafitiwa walishirikishwa bila kushurutishwa.

**1.7Ufafanuzi wa Istilahi.**

| | |
|---|---|
| **Dhima** | : Kiini cha matukio miongoni mwa jamii. |
| **Mawazo ganda** | : Mawazo ambayo yanalenga kuikejeli na kuidunisha jamii. |
| **Rabsha** | : Mitafaruku, malumbano na vita kati ya jamii. |
| **Uneni** | : Mazungumzo yasiri/faraghani miongoni mwa jamii. |
| **Urejelezi** | : Diskosi ama Lugha inayotumiwa hasa kwa njia fiche na inalenga kuikejeli nakuidunisha jamii hasa wakati wa vita na vurugu, na pia wakati wa amani kwa matumizi ya lugha ama neno. |
| **Vurugu** | : Kutokuwa na amani, hali ya jamii kuwa na malumbano; ugomvi, fujo, vita kati ya jamii. |

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sehemu hii imegawanywa katika sehemumbili. Sehemu ya kwanza inawasilisha maandishi yaani, tafiti na maelezo mbalimbali. Sehemu ya pili inaangazia misingi ya nadharia.

## 2.2 Mapitio ya Maandishikuhusu Urejelezi miongoni mwa Jamii mbalimbali

Mapitio ya maandishi yamefanywa kwa mtindo wa kimada na kuangazia dhana ya matumizi ya lugha ya urejelezi na mahusianokati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis. Stell na Fox (2014) walichunguza kategoriaza makabila na kategoria nyingine kama vile ujio wa makabila mengine na namna kategoria hizi zinavyoathiri maingiliano kimawasiliano nchini Namibia. Waligundua kuwa mawazoganda yanapatikana miongoni mwa washiriki wa utafiti huo. Washiriki walipendelea kujihusisha na watu wa kabila lao ambao kama vileMaori na Pakeha (white New Zealander), Herero, Ovambo, Nama na Damara. Pia kuna matumizi ya lugha rejelezi ambayo ilitumiwa kuwarejelea watu wa makabila mengine na kuwaweka katika kategoria. Washiriki walionyesha kuwa watu hujaribu kukwepa na kukataa sifa wanazopewa na watu wa makabila mengine.

Kulingana na Stell na Fox (2014), lugha ya urejelezi iliyotumiwa ilikuwa kwa misingi ya rangi; uweusi na uweupe. Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano na mbinu ya mazungumzo ambapo alinukuu yaliyojiri na kupata deta ya utafiti huo. Mtafiti alitumia mahojiano ya vikundi na kuwapa watafitiwa fursa ya kujadili mada husika, deta ya maoni, mitazamo na mielekeo ilipatikana kwa urahisi kwa kibinafsi na zilielezewa hadharani miongoni mwa makundi (Dornyei, 2007). Mtafiti alinasa yaliyojiri, wanavyohisi na namna wanavyotenda (Oliveira na wenzake, 1998). Mahojiano yalinukuliwa na yaliyojiri yalirekodiwa kwa kutumia kinasa sauti na kukusanya deta. Deta ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo ambapo watafiti walishirikishwa. Utafiti huo unathibitisha kuwa rabsha na kutoelewana kati ya makabila mbalimbali miongoni mwa jamii hutokea kutokana na matumizi ya urejelezi. Pia utafiti huo ulidhibitisha kuwa urejelezi hutumiwa na watu wa kabila au kundi moja kuwarejelea watu wa kabila/kundi lingine. Kama amabvyo nadharia ya utambulisho wa makabila/mbari inavyo angazia. Tofauti ya utafiti huo na utafiti huu ni kuwa utafiti huuulikuwa

unaangaziaurejelezi na mahusiano ya jamii hizi kwa misingi ya makundi mawili tofauti Abagusii na Kipsigis nchini Kenya (Agheyisi & Fishman, 1970).

Utafiti huo uliangazia kabila kwa misingi ya rangi ilhali utafiti huu uliangazia kabila kwa misingi ya urejelezi. Utafiti huo unasaidia kuelewa kwamba kuna matumizi ya lugha ambapo mawazo ganda yapo miongoni mwa washiriki. Washiriki hupendelea kujihusisha na watu wa kabila lao Kama amabvyo nadharia ya utambulisho wa makabila/mbari inavyo angazia.

Kazi hii ya watafiti hawa inasaidia kazi hii ya sasa kuonyesha kwamba jamii hujaribu kukwepa na kukataa sifa wanazopewa na watu wa makabila mengine na hivyo kuzua malumbano hasa miongoni mwa jamii zinazopakana. Utafiti wao ulisaidia mtafiti kuelewa kuwa jamii hujitenga na jamii nyingine tofauti na wao, kwa kuwa kuna matumizi ya urejelezi ambayo jamii hutumia dhidi ya jamii nyingine ambayo haikubaliki miongoni mwa jamii nyingine.

Lugha na muktadha ninjia kuu ya kuonyesha utambulisho kwa ujumla na ni mahususi (Drew, 1998; Zienkowski, 2011). Kwa hiyo, lugha huonyesha mambo mengi katika mipaka ya kijamii, ambayo huelezwa kwa misingi ya ishara zinazoonekana katika viwango tofauti vya matumizi ya lugha. Kwa sababu ya sifa tofauti, ishara hizi zimejenga misingi ya utafiti katika mikabala tofauti tofauti kinadharia. Maoni ya wataalam hawa yanasaidia utafiti huu kujenga misingi yake ya utafiti wake. Ishara zinazoangaziwa katika utafiti huu ni urejelezi jamii ya Abagusii na Kipsigis hutumia. Urejelezi hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine.

Guillem (2017), mtafiti kutoka chuo kikuu cha Valencia, nchini Argentina aliangazia uhusiano kati ya mazoea fulani ya lugha ya urejelezi na mifumo ya kiitikadi kwa upana wa msingi ya rangi na ubaguzi wa rangi. Aligundua kuwa kuna urejelezi ambao huzua ukosefu wa usawa miongoni mwa jamii. Katika kazi yake aligundua kwamba matumizi ya urejelezi kila siku na katika taasisi, yalionyesha ruwaza za kuzungumza ambapo wazungumzaji walitoa maneno yanayoonyesha itikadi kuhusu makundi tofauti tofauti. Baadhi ya matumizi ya urejelezi yalionyesha mikakati ya “wao” na “sisi”. Anahitimisha kwa kusema kuwa urejelezi huu unaonyesha itikadi dhidi ya makundi mengine yanayosababisha ubaguzi wa rangi na hukwepa kupigiwa msasa na hivyo kuendeleza mitafaruku kati ya watu wenye rangi tofauti. Utafiti huo unaonyesha jinsi urejelezi unavyoweza kuendeleza ubaguzi na ukosefu wa amani miongoni mwa jamii. Mtafiti anatumia mbinu ya kushiriki ambapo mjadala unazuliwa na watafitiwa

wanashiriki katika mjadala huo ambapo walitoa mawazo yao. Sawa na utafiti huu ambao mtafiti alichunguza urejelezi miongoni mwa jamii ya Abagusii na Kipsigis. Hata hivyo, utafiti huo uliegemezwa katika rangi ya wanadamu ilhali Utafiti huu ulichunguza matokeo ya matumizi ya urejelezi katika mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis.

Kwa kurejelea ruwaza za mwingiliano kiutamaduni kila siku, Elchinova (2001), alichunguza njia mbalimbali ambazo wananchi wa Bulgaria walijaribu kusuluhishuia rabsha, vurugu na kutoelewana miongoni mwa jamii zao. Alijaribu kutoa taswira ya hali ya makabila nchini Bulgaria, kwa kuangazia makabila matatu makuu ambayo yanajitambulisha kwa misingi yao ya dini. Aliangazia uundaji wa kimazungumzo na maelezo ya utambulisho katika matumizi ya lugha kila siku. Aligundua kuwa kuna maumbo mbalimbali ya urejelezi wa kutengwa na kuletwa pamoja iliyojitokeza katika utamaduni kila siku, hii inachangia katika kuhifadhi usawa katika mahusiano kati ya makabila. Aligundua kwamba mikakati na kaida za mahusiano haya yanategemea vipengele mbalimbali.

Utafiti wa Elchinova ulisaidia utafiti huu katika kuelewa kuwa wanajamii wanatambua tofauti zilizopo kati yao kwa msingi wa dini. Tofauti hizi huweza kuleta rabsha, vurugu na kutoelewana kupitia kwa matumizi na urejelezi unaotumiwa. Utafiti huu pia unaonyesha kuwa wanajamii wanapogundua matumizi ya urejelezihuleta kutoelewana kati yao, hujaribu kutafuta namna ya kusuluhisha rabsha, vurugu na kutoelewanakati yao. Utafiti huu uliangazia tofauti ya wanajamii kwa msingi wa tofauti za kidini ilhali utafiti huu wa sasa uliangazia wanajamii wanaotofautiana kwa msingi wa lugha yao na utamaduni wao. Utafiti huo ulisaidia utafiti huu, kuwa jamii hutofatuana kwa nyenzo mbalimbali. Kwa hiyo utafiti huu ulichunguza matokeo ya matumizi ya urejelezi katika mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis.

Kang (2004), alionyesha jinsi washauri wa kambi ya Korea Marekani walivyojenga utambulisho wa kikabila kwa kujitabakisha katika lugha, kama ambavyo nadharia ya utambulisho wa lugha za kikabila inayohusu makabila/mbari za binadamu na mahusiano kati ya jamii inavyodokeza. Kujitambulisha kikabila kulimuweka mshauri katika hadhi fulani iliyolingana na madhumuni ya kibinafsi ya washauri hao katika kambi ya Korea Marekani. Anaeleza kuwa washauri hawa walijitambulisha kwa misingi yatabaka lao huku wakionyesha mitazamo yao kuhusu nani wafao zaidi kuwa katika ile kambi na motisha yao binafsi ya kuwa

pale. Pia wanajitabakisha kwa kusema wao ndio “Wakorea Wamarekani bora zaidi” wanaostahili kuwa katika ile kambi. Hata hivyo, kazi hii haionyeshi dhana ya rabsha, vurugu na kutoelewana ila inaonyesha namna ambavyo wazungumzaji hujipendelea wao wenyewe kwa misingi ya kikabila jambo ambalo hutokea katika mazingira ya wingi lugha na huenda ikawa hatari, kama ambavyo nadharia ya utambulisho wa makabila/mbari inavyo angazia. Kazi hiyo imesaidia kuonyesha namna urerejelezi unavyotumiwa kwa kujipendelea. Ikiwa matumizi ya urejelezi yanaweza kutumiwa kwa kujipendelea, basi yanaweza kutumiwa kukejeli au hata kumrejelea mtu mwingine. Utafiti huu wa sasa ulichunguza matokeo ya matumizi ya urejelezi katika mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis.

Urejelezi wa kijamii huzuka paleambapo mhusika mmoja ama zaidi huwa na nia ya kutoelewana ilikutekeleza yale ambayo wanahitaji kutekeleza dhidi ya jamii nyingine ambapo urejelezi hutumiwa kuirejelea jamii husika (Wolff, 2006). Hii ni sawa na ambavyo nadharia ya utambulisho wa lugha za kikabila inayohusu makabila/mbari za binadamu na mahusiano kati ya jamii inavyoangazia. Ni kutokana na hali hii ambapo rabsha na vurugu miongoni mwa jamii dhidi ya jamiinyingine huzuka, kwani rabsha inapotokea kutokana na matumizi ya urejelezi huu kila mmoja hukimbilia jamii yake. Maoni haya yalisaidia utafiti huu katika kuelewa misingi ya tofauti za kikabila kati ya jamii. Pia yalisaidia utafiti huu kuelewa misingi ya tofauti katika jamii. Hata hivyo, utafiti wake unatafoautiana na utafiti huu kwa kuwa utafiti huu uliangazia jamii ya Kipsigis na Abagusii.

Wataalamu hawa wametoa maelezo kuhusu rabsha, vurugu na kutoelewana kati ya jamii inayozuliwa na matumizi ya urejelezi. Wameonyesha jinsi matumizi haya yanavyozua rabsha vurugu na vita miongoni mwa jamii mbalimbali na athari zao. Hata hivyo, tafiti hizi zinaangazia rabsha na vurugu inayozuliwa na lugha inayoonyesha ubaguzi wa rangi. Utafiti huu ulichunguza matokeo ya matumizi ya urejelezi katika mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis. Nyukuri (1995) aliangazia vurugu na rabsha kutokana na vita vya kikabila katika pembe ya Afrika hasa Somali, Ethiopia, Rwanda na Sudan na Sudan Kusini. Anapendekeza jinsi ya kuleta suluhu na kusema kuwa rabsha na vita hivi vinatokana na matukio ya kihistoria, kuhama miongoni mwa jamii mbalimbali, uhaba wa rasilimali, uchumi, siasa na matukio mengine mbalimbali ya kijamii. Hata hivyo, utafiti huohaukuangazia jinsi ambavyo urejelezi unavyozua vurugu, kutoeleana na rabsha miongoni mwa jamii. Pia utafiti huu uliangazia jamii

za pembe za Afrika. Utafiti huo ulisaidia katika kuelewa visababishi vya rabsha na vurugu miongoni mwa jamii. Utafiti huu wa sasa, kwa upande wake ulichunguza matokeo ya matumizi ya urejelezi katika mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigisnchini Kenya.

McOnyango (1995) anaelezea kuhusu dhana ya kutoelewana, rabsha na vurugu miongoni mwa jamii za Kiafrika na kudai kuwa hili sio tukio la kijamii la kisadfa ambalo linatokokana na mipaka tu. Kulingana na McOnyango kutoelewana, vurugu na rabsha baina ya jamii, inatokana na kinyongo cha kiasili dhidi ya jamii moja. Anatoa mifano ya vurugu, rabsha na vita miongoni mwa jamii ya nchi kama vile Rwanda, Burundi, Mashariki mwa Afrika na Somali katika pembe la Afrika ambapo kuna makabila mawili na wengine ni jamii moja. Vilevile anadokeza kwamba wataalam mbalimbali hushughulikia rabsha baina ya jamii bila kuangalia matukio haya kwa undani. Anasema kwamba uonevu wa kijamii, kiuchumi na kisiasa umekita mizizi miongoni mwa jamii za Kiafrika. Utafiti huo ulishugulikia suala la rabsha, vurugu na kutoelewana dhidi ya jamii kwa ujumla. Matokeo yake yanatofautiana na utafiti huu kwa kuwa utafiti huu ulilenga kuchunguza matokeo ya matumizi ya urejelezi katika mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis. Utafiti huo unachangia utafiti wa sasa kwa kudhibitisha kwamba suala la matumizi ya urejelezi lipo ila halijachunguzwa. Hivyo basi, utafiti huu wa sasa umechunguza kwa undani suala hili.

Maelezo ya watafiti hawa yalisaidia utafiti huu kupata msingi bora. Pia utafiti huu unapata kuelewa dhana urejelezi inayozua rabsha, vurugu na kutoelewana miongoni mwa jamii mbalimbali zinazopakana. Tafiti hizi zinaangaziamadhara haya kati ya jamii ulimwenguni. Hata hivyo, tafiti hizo hazikuangazia matumizi ya lugha kwa misingi ya urejelezi. Utafiti huu ulichunguza matokeo ya matumizi ya urejelezi katika mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis.

Muriungi na Mukuthuria (2016), wanaangazia matumizi ya urejelezi bungeni kati ya viongozi wa jamii mbalimbali. Wanadokeza kwamba urejelezi ni sehemu pana inayorejelewa na inayozua maana tofauti miongoni mwa jamii. Wataalam hawa waliangazia matumizi ya urejelezi; inayotumika bungeni na viongozi nchini Kenya. Kulingana na wao, urejelezi huu huzua chuki, vurugu na rabsha. Watafiti hawa walishiriki vikao bungeni na walitumia mbinu ya kuchanganua, kukagua, kuweka deta inayokusanywa waziwazi na kurekodi katika viwango

mbalimbali. Maoni ya Muriungi na Mukuthuriayalisaidia utafiti huu katika kuelewa misingi ya matumizi ya kurejeleana miongoni mwa jamii. Pia yalisaidia utafiti huu kuelewa tofauti za kijamii. Hata hivyo utafiti wao uliangazia urejelezi bungeni ilhali utafiti huu unamulika matokeo ya matumizi ya urejelezi katika mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis unaozua kutoelewana, rabsha na vita kati yao katikamaeneo ya Borabu na Chebilat mpaka wa jamii hizi mbili Kaunti ya Nyamira na Bomet.

Langat  na wenzake (2017) walitafiti chanzo cha rabsha, vurugu na kutoelewana kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis na viwango vinavyoleta amani katika mipaka ya Chebilat na Borabu jimbo la NyamiranaBomet. Kulingana nao, jamii hizi mbili zimekuwa katika hali ya vurugu, rabsha na kutoelewana. Serikali, asasi za kiraia na jamii ya mitaa wametia juhudi kuletasuluhu na kujenga amani kati ya jamii hizi bila kufua dafu. Waligundua kuwa wizi wa ng'ombe, mabishano ya mipaka, siasa, shauku kati ya wanajamii na vijana wasio na kazi walizua rabsha na vurugu kati ya jamii hizi. Walipendekeza kuwa juhudi za kujenga amani na kuleta suluhu kati ya jamii hizi mbili zinapaswa kuendelezwa na kuimarishwa kwa asasi za kijamii. Utafiti huo ni ithibati kwamba kuna kumbukumbu za kutoelewana miongoni mwa jamii kwani kuna ithibati kuwa kuna rabsha, vurugu na kutoelewana kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigisna zinatambuliwa. Watafiti hawa waliangazia vyanzo vya rabsha, vurugu na kutoelewana huko. Utafiti huo uliangazia chanzo cha rabsha na vurugu hizo kwa ujumla. Ingawa utafiti wao uliangazia chanzo cha vurugu na kutoelewana, suala la urejelezihalikuwa kipaumbele kwaokama utafiti huu ulivyodokeza, kwaniutafiti huu ulichunguza matokeo ya matumizi ya urejelezi katika mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis. Utafiti wa Langat na wenzake ulisidia utafiti huu kuelewa kuwepo kwa vyanzo vya rabsha, virugu na mitafaruku kati ya jamii mbalimbali.

Odongo (2009) alichunguza namna jamii ya Luo, Abagusii na Kipsigis wanavyoishi katika eneo la Sondu.Eneo hili lina jamii hizi tatu na linajulikana kwa umaarufu wa soko ambalo linatumiwa na jamii hizi tatu. Hata hivyo eneo hili huwa na kutoelewana kati ya jamii hizi tatu inayosababishwa na siasa na uhaba wa rasilimali. Waligundua kwamba wakati wa siasa, jamii hizi huwa narabsha na vitakati yao. Pia waligundua kuwa mitazamo ya kikabila katika eneo hili hufungamana na mawazo ganda. Mawazoganda ambayohuzua uhasama kati ya jamii hizi. Kulingana na wataalam hawa biashara na ukulima ni baadhi ya shughuli ambazo zinawasaidia

kuishi kwa amani. Shughuli nyingine zinazounganisha jamii hizi ni pamoja na ndoa za mseto, michezo, harusi, matanga na jando. Utafiti huo wa Odongo ulisaidia utafiti huu kuelewa jamii ya Abagusii na Kipsigis na hali ya maisha yao kwa jumla. Hata hivyo utafiti huo haukuangazia urejelezi kati ya jamii hizi, bali namna wanavyoishi kwa pamoja ijapokuwa pana utofauti wa kabila. Pia utafiti huo uliangazia jamii tatu Luo, Kipsigis na Abagusii. Utafiti huu kwa upande wake ulichunguza matokeo ya matumizi ya urejelezi katika mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis.

Nyagosia (2017) alichunguza mwingiliano, utangamano na utumizi wa nguvu za kijeshi kati ya Abagusii na majirani zao katika vipindi vya kabla ya wakoloni, wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Alitathmini utangamano wa Abagusii na majirani zao kwa misingi ya mabadiliko kihistoria. Aligundua kuwa kuna mahusiano chanya kati ya Abagusii na majirani zao ambao ni Luo, Masaai na Kipsigis. Aidha, aligundua kuwa wakati huo huo kulikuwa na rabsha na vurugu kati ya Abagusii na majirani zao. Rabsha hizizilionekana kupitia vita na wizi wa mifugo. Alipendekeza kuwa serikali inapaswa kuingilia kati ili kuhakikisha kuwa jamii ya Abagusii na majirani wao wanaishi kwa amani. Kupitia utafiti wa Nyagosia, utafiti huu wa sasa unafaidika kwa maarifa ya kihistoria kuhusu rabsha, vurugu na mitafaruku kati ya jamii ya Abagusii na majirani wao, hasa Kipsigis. Utafiti huo ulijifunga upande wa Abagusii, pia kigezo cha urejelezi hakikuangaziwa. Kwa hivyo, utafiti huu wa sasa utaangaziamatokeo ya matumizi ya urejelezi katika mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis.

Kazi ya Nyagosia iliangazia jamii ya Abagusii na Kipsigis na hali ya mahusiano yao. Tafiti hizi zilisaidia kazi hii kudhibitisha uwepo wa kutoelewana vurugu na rabsha kati ya jamii hizi (Nyagosia, 2017). Pia tafiti hizi zinajenga msingi wa utafiti huu wa sasa kwa kuweka jamii hizi mbili katika taswira ya historia. Hata hivyo watafiti hawa hawakuangazia mahusiano ya jamii hizi mbili kutokana na urejelezi na ikiwa urejelezi huu unachangia katika vurugu au uwiano. Hii huenda ni kwa sababu suala la urejelezihalikuwa katika upeo na mipaka ya tafiti zao. Kwa misingi hiyo basi, utafiti huu uliangazia mahusiano ya jamii ya Abagusii na Kipsigis kwa kuchunguzamatokeo ya matumizi ya urejelezi katika mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis.

## 2.3 Misingi ya Nadharia.

Utafiti huu uliogozwa kimsingi na Nadharia ya Utambulisho wa Lugha za Kikabila inayohusu makabila/mbari za binadamu na mahusiano kati ya jamii, yaani 'Ethnolinguistics identity theory, (ELIT). Sapir (1992) ndiye mwasisi mkuu wa nadharia hii (Wolff & Holmes, 2011). Wahitifaki/wachangizi wengine wa nadharia hii ni Haugen (1966), Giles na wenzake (1987), Haugen (1972), ni baadhi ya waasisi waandamizi wa nadharia hiiya utambulisho wa lugha inayohusu makabila/mbari za binadamu inayohusu maelezo ya kisayansi kuhusu mila na tamaduni za kijamii ambapo jamii ina dhana ya ubinafsi miongoni mwao na mahusiano ambayo jamii moja inayo dhidi ya jamii nyingine. Nadharia hiiinaangalia mahusiano kati ya jamii mbalimbalina jinsi ambavyo jamii moja inalenga kutumia semi kati yao dhidi ya jamii nyingine ambazo wanachukulia kuwa duni na ambazo zinawalenga wao. Inajikita kwa misingi ya ubinafsi wa kijamii ambapo jamii inajiangalia kwa misingi ya itikadi, mila na tamaduni zao kama jamii inaoyoongea lugha moja (Giles & Johnson, 1987). Nadharia hii inahusu uhusiano wa lugha ambayo ni asasi za jamii za lugha husika na inajikita katika nguzo nne kuu.

Utambulisho wa kijamii, ambapo jamii inajitambua kuwa wao ni jamii tofauti na jamii nyingine na hivyo basi wanajitenga kijamii. Nguzo hii ilitumiwa kuonyesha istilahi na misamiati ya kiurejelezi inayotumiwa na Kipsigis kuwarejelea Abagusii na ile inayotumiwa na Abagusii kuwarejelea Kipsigis. Pia nguzo hii ilitumiwa kuelezea istilahi hizo za kiurejelezi kwa mtazamo wa kila jamii kivyake.

Jamii moja hujilinganisha na jamii nyingine kwa lengo la kuonyesha  kuwa wao ni bora zaidi, wakilinganishwa na jamii nyingine ambazo ni jirani zao, hali hii ni wazi kwa kuwa urejelezi ambao jamii moja inatumia dhidi ya jamii nyingine mara nyingi una nia ya kuidunisha na kuikejeli jamii nyingine ambapo hali hii huzua rabsha vurugu na vita dhidi ya jamii nyingine hasa jamii zinazopakana.

Nadharia ilitumiwa kuelezea athari ya urejelezi inayotumiwa na jamii ya Abagusii na Kipsigis kurejeleana, na ndio iliyoongoza utafiti huu katika kuchunguza urejelezi uliyotumiwa na jamii hizi mbili kurejeleana, iliathiri vipi utangamano na mwingiliano wa jamii hizi mbili katika maisha yao ya kila siku.

Mipangilio ya kijamii na jinsi ambavyo jamii inatekeleza majukumu yake kama jamii mojahasa

baada ya mitafaruku kati yao na jamii nyingine (Kenpointner, 2005). Nguzo hii iliongoza utafiti huu katika kuchunguza mapendekezo ya suluhisho ya amani katika utangamano wa Kipsigis na Abagusii. Ikiwa lugha ya urejelezi ina athari hasi kwa utangamano wa jamii hizi mbili, basi wao hufikia vipi suluhisho ili kuendeleza mahusiano ya amani kati yao, hasa kwa sababu kuna baadhi ya rasilmali wanayotumia kwa pamoja. Mifano ya rasilimali hii ni kama vile *mito*, misitu na soko na hata maeneo ya burudani ambapo wao hushiriki pamoja. Pia kuna matukio ya ndoa kati yao ambapo hurejeleana kwa kutumia majina kama *Kamama, bomori, batieb* kutokana na ndoa kati ya watoto wao kwa upande wa jamii ya Kipsigis, ilihali miongoni mwa jamii ya Abagusii kuna matumizi ya urejelezi kama vile *Omosani, korera, minto, bamwabo* yanaonyesha rafiki na mtu wa karibu sana, matumizi ya korera kutokana na ndoa kati ya watoto wao ni urejelezi muhimu sana kwa kuwa urejelezi hii unaleta jamii pamoja. Hali hii huonyesha hali ya amani na utegamano kati ya jamii hizi mbili. Hivyo, namna wanavyoafikia utangamano ingawa wanatumia lugha ya urejelezi ambayo wakati mwingine huwa hasi ilichunguzwa na kuafikiwa kupitia nadharia hii.Tofauti za kijamii za kisaikolojia, ambapo jamii moja inajiona kuwa wao ni bora kuliko jamii nyingine.

Nadharia hii inalenga makabila; mipaka ya jamii; na utambulisho wao kama jamii. Nadharia hii ni mwafaka katika utafiti huu kwa kuwa inakidhi na kuafiki mahitaji ya utafiti huu ambao ulichunguza matokeo ya matumizi yaurejelezi katika mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti ametoa maelezo ya mbinu zilizotumiwa katika kukusanya na kuchanganua deta ya utafiti. Sura hii imeangazia ukusanyaji na uchanganuzi wa deta. Sehemu ya kwanza ni muundo wa utafiti. Hii ni kwa sababu muundo wa utafiti hushikilia sehemu nyingine zote za mbinu za utafiti kama vile: mahali pa utafiti, umma uliolengwa kuhusishwa katika utafiti huu, uteuzi wa sampuli na mbinu za ukusanyaji deta zimeangaziwa. Katika kujadili mbinu za ukusanyaji deta, maelezo ya jinsi deta ilivyofikiwa na kuelezewa yamedokezwa katika sehemu hii. Maelezo ya uzingatiaji wa maadili ya utafiti vilevile yametolewa.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ni wa kithamano mkabala wa uchanganuzi usemi. Utafiti wa kithamano husaidia kuelewa na kueleza tajriba ya watu na jambo mahususi kuhusu watu wanaotafitiwa (Howlett na wenzake, 2014). Utafiti wa kithamano humfahamisha mtafiti kuelewa maswala ya jamii na matatizo ya binadamu (Creswell, 1998). Mtafiti huchanganua maneno, ripoti, maoni ya watafitiwa na kutekeleza utafiti katika mazingira asilia. Data ya utafiti wa kithamano huzua maelezo ya nyanjani alizonukuu mtafiti, kanda za sauti, mahojiano na nyaraka (Creswell, 2009; Merriam, 2009). Kwa hivyo utafiti huu ni wa kithamano kwani deta ya utafiti huu ulikuwa mazungumzo kati ya mtafiti na watafitiwa.

## 3.3 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulifanyiwa nyanjani. Mtafiti alifanya utafiti wake katika maeneo ya Sotik- Borabu, hasa katika maeneo ya tarafa ya Ndanai, kata ya Gelegele na kata ya Esise, tarafa Borabuambapo ni mpaka wa jamii ya Abagusii na Kipsigis. Maeneo haya yaliteuliwa kimakusudi kwasababu ni mipaka ya jamii ya Abagusii na Kipsigis ambapo kumekuwa na mitafaruku, vurugu narabsha zisizoeleweka ambazo mtafiti alichunguza katika utafiti huu. Maeneo haya pia yaliteuliwa kwa sababu hali zote zinazotafitiwa zinapatikana katika maeneo hayo.

### 3.4 Umma lengwa

Umma uliolengwa kuwa sampuli ya utafiti huu niAbagusii na Kipsigiswanaoishi tarafa ya Ndanai, kata ya Gelegele na kata ya Esise, tarafa Borabu ambapo ni mpaka wa jamii hizi mbili. Uteuzi huu ni mwafaka kwa kuwa watafiwa hawa wana uelewa wa matukio ambayo yamekuwa yakisababisha kutoelewana, mitafaruku, vurugu na vita kati yaonakuwa wanaishi maeneo haya kwa kipindi kirefu. Sampuli hii iliteuliwa kimakusudi kupitia msaada wa viongozi wa maeneo yaliyoteuliwa katika utafiti huu. Maswali ya utafiti yalielekezwa kwa vikundi viini vilivyoteuliwa kutokana na umma lengwa kutokana na maswali ya Nadharia ya utambulisho wa lugha za kikabilaza binadamu (‘Ethno-linguistics Identity Theory (ELIT)) na mahusiano kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis.Utafiti uliteua vikundi hivikwa sababu hawa ni watu wanaishi maeneo haya na hivyo wanauelewa na kuna uhusiano wa karibu baina ya jamii hizi mbili. Sampuli hii pia ilikuwa ni kiwakilishi cha jamii nzima kutokana na kuishi kwao katika eneo lile kwa muda mrefu na kwa sababu wanatoka katika jamii hizi mbili.

### 3. 5 Uteuzi wa Sampuli

Kwa minajili ya utafiti huu uteuzi wa sampuli ni Abagusii na Kipsigis wanaoishi eneo la Borabu - Sotikkata ya Gelegele na kata ya Esise, tarafa Borabu ambapo ni mpaka wa jamii hizi mbili. Sampuli iliyoteuliwa ni wanaume wazee 10 na kina mama wazee wenye miaka 60 na zaidi kutoka pande zote za Abagusii na Kipsigis na vijana 10 kutoka pande zote za Abagusii na Kipsigis wenye umri wa miaka 24 hadi 35. Watafitiwa 30 kutoka pande wa Abagusii na Kipsigis.Utafiti huu ni wa mfano (Creswell, 1998) anaelezea kuwa katika utafiti wa mfano, Watafitiwa wanafafanuliwa kama ni watafitiwa walio na mitazamo iliyo sawa. Mtafiti alitumia watafitiwa hawa kupata mawazo yao kulingana na kusudio la utafiti. Hii ni kwa sababu jamii hizi zinatumiwa tu kama mfano miongoni mwa jamii nyingine nyingi na mifano mingi. Mtafiti huchagua jamii anayokusudia kufanya utafiti kimakusudi miongoni mwa jamii nyingine mbalimbali. Uteuzi wa kimakusudi ni chaguo la watafitiwa kwa sababu ya sifa ambazo watafitiwa walio nayo na hali zinazotafitiwa (Tongco, 2007). Kwa misingi ya maelezo haya, uteuzi wa jamii hizi mbili kuna sifa na hali zinazotafitiwa katika utafiti huu kwani haya ndio maeneo ambayo yamekuwa na rabsha mitafaruku na hata vita visivyoeleweka miaka hadi miaka.

Kama asemavyo Patton (2002), mantiki na nguvu ya uteuzi wa kimakusudi imo katika kuchagua eneo lenye ukwasi wa deta ili kupata uelewa wa undani. Uteuzi wa kimakusudi imechukuliwa kuwa ni suluhisho za vizuizi vya muda, raslimali, ufikiaji wa deta au habari na utaalamu (Benoot na wenzake, 2016; Patton, 2002). Uteuzi wa kimakusudiutumiwa kutafiti maoni ya watu wenye tajriba fulani. Mbinu hii ni muhimu kwa kuwa watafiwa hutangamana bila kuwa na shauku na wao hupeana motisha ya kutoa mawazo yao bila kuwa na woga.

Matumizi ya mbinu hii ilimpa mtafiti wakati rahisi kupata deta kwa gharama ya chini. Pia ilikuwa rahisi kuwasiliana na watafitiwa na kuchanganua deta ambayo ilikusudiwa. Mtafiti aliwasiliana na watafitiwa moja kwa moja na deta iliyokusanywa ilitumiwa kupitia mawazoya watafitiwa.

Mtafiti aliteua baadhi ya watafitiwa miongoni mwa jamii hizi ili kuwafanyia mahojiano ya moja kwa moja. Aidha, mtafiti alitumia mbinu ya mazungumzo ambapo alinukuu yaliyojiri. Katika uteuzi huu, mara nyingi watafitiwa huwa hawafahamiani, ila wao huwa na mitazamo sawa. Mbinu hiiilitumiwa baada ya vita vya dunia vya pili ili kuchanganua maoni ya wasikilizaji katika vipindi vya radio (Stewart & Shamdasani, 1990). Tangu wakati huo wataalum wa sayansi ya kijamii wamekuwa wakitumia mbinu hii katika tafiti mbalimbali ilikubaini mawazo na fikira za jamii kupitia watafitiwa. Kwa sababu mtafiti hakuwa na umilisi wa lugha ya Kipsigis, ilikuwa vigumu kufanya mahojiano kikamilifu na yenye kuzua deta bora. Kukabiliana na hili, mtafiti kupitia chifu, alipata kijana wa Kipsigis, aliyemsaidia kuzungumza na wanajamii wa Kipsigis wakati wa mahojiano katika vikundi viini ili kupata deta aliyoitaji.

### 3.6 Ukusanyaji wa Deta

Mbinu zilizotumiwa kukusanya deta ya utafiti huu ni ethnografia. Ethnografia ni mbinu inayochanganya maelezo na uchambuzi wa jamii fulani na maelezo na uchanganuzi wa lugha (Smart, 2012). Vilevile huhusisha kueleza na kufasili utamaduni au kikundi fulani katika jamii au mfumo fulani (Howlett na wenzake, 2014). Hii ni mbinu ya ukusanyaji deta ambayokikundi cha watu wanaotumia pamoja rasilimali za lugha na kaida za maingiliano, usemi na ufasiri ambapo uchunganuzi-shiriki na mahojiano ya vikundi vilivyoteuliwa kimakusudihushirikishwa. Katika matumizi ya mbinu hii mtafiti hushiriki katika shughuli za kila siku za kikundi hicho kwa kutumia mbinu ya mahojiano na utazamaji-shiriki. Ethnografia

huweza kufanywa mahali popote pale huku mtafiti akitazama na kurekodi matokeo ya majadiliano kadri muda unavyosonga (Sangasubana, 2011).

Mtafiti alifanya mazungumzo na watafitiwa ambapo alinukuu yaliyojiri nakupata deta ya utafiti. Mahojiano hayo yalikuwa ya kibinafsi na vilevile katika vikundi vya kina Baba wazee, kina mama na vijana hasa waendeshao pikipiki (boda boda) kutoka jamii zote mbili. Hii ni kwa sababu lugha wanayotumia wazee na kinamama ni tofauti na lugha ya vijana. Aidha vijana huhusika sana katika vurugu, vita na rabsha miongoni mwa jamii ukilinganisha na wazee kwa kuwa wao ni barubaru na wana nguvu. Mahojiano ya vikundi yalihusisha kuwaleta watafitiwa pamoja kujadili mada aliyopanga mtafiti. Mtafiti alitumia mahojiano ya vikundi na kuwapa watafitiwa fursa ya kujadili mada husika, deta ya maoni, mitazamo na mielekeo ilipatikana kwa urahisi kwaubinafsi ambapo ilielezewa hadharani miongoni mwa makundi (Dornyei, 2007). Mtafiti alinasayaliyojiri kulingana na Oliveira na wenzake (1998), wanaongezea kuwa mahaojiano ya vikundi hutoa habari kuhusu kile watu wanafikiria, wanavyohisi na namna wanavyotenda. Mahojiano yalinukuliwa nayaliyojiri yalirekodiwa kwa kutumia kinasa sauti na kukusanya deta. Katika kukusanya deta hii ilibidi mtafiti awafahamishe watifiwa hali hii.

### 3.7 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Deta

Katika hatua hii mtafiti alidondoa deta inayohusiana na urejelezi kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis katika matini yaliyonukuliwa. Deta iliyokusanywa ni matokeo ya matumizi ya lugha ya urejelezi. Uchunguzi na uwasilishaji wa deta hunakili matukio, kurekodi kwa kutumia ukanda na kurekodi bila picha au video na kuuliza maswali ambayo yanalenga kuweka wazi mazungumzo kati ya watafitiwa husika (Guest na wenzake, 2013), uchunguzi na uwasilishaji wa deta huweka wazi, hurahisisha upatikanaji na ugunduzi wa maana ambapo watu hutumia kuunda mantiki ya maisha yao ya kila siku (Jorgensen, 1989) kuwa mtafiti hushiriki na kutazama hali za maisha ya kila siku ya watu husika. Anaeleza kuwa mtafiti lazima awe na juhudi kuhakikisha kuwa amepunguza kiwango cha kuvuruga na kuingilia washiriki kama mgeni au mshiriki asiyehusika katika hali inayotafitiwa. Hii lilikuwa muhimu hasa katika muktadha wa utafiti huu, Kule kushiriki kulimpa mtafiti fursa ya kufanya mahojiano na watafiti bila kuwa na tashwishi yoyote (Fox, 1998; Jorgensen, 1989).

Mpangilio maalum wa uchanganuzi wa deta ya utafiti huu ni kama ufuatao:

Mtafiti alinukuu deta yote aliyokusanya iliyofaa mada ya utafiti. Mazungumzo yote kati ya jamii zote mbili yalinukuliwa jinsi yalivyo kwa kutumia kinasa sauti. Mazungumzo yaliwekwa katika maandishi yawe matini huku kila urejelezi ukiambatanishwa na mzungumzaji wake kwa usahihi. Majina yametumiwa katika ukusanyaji wa deta hii. Hata hivyo majina hayo si majina yao halisi wanayotumia katika maisha yao ya kila siku. Majina hayo yalibuniwa kutegemea jamii/kabila aliyotoka mshiriki. Kwa mfano, iwapo mshiriki alitoka jamii ya Abagusii au Kipsigis, majina yao yalibuniwa kuonyesha asili hiyo.

Katika hatua ya Udondozi, mtafiti alidondoa deta inayohusiana na lugha ya urejelezi katika matini yaliyonukuliwa. Mtafiti alidondoa matini inayohusiana na mazungumzo ya lugha ya urejelezi miongoni mwa jamii hizi kwa deta yote iliyokusanywa. Pia, ni katika hatua hii ambapo mtafiti alidondoa deta iliyokuwa mwafaka zaidi na yenye ukwasi na iliyojibu maswali ya utafiti kwa ubora zaidi. Mtafiti alibainisha deta iliyodondolewa kulingana na malengo ya utafiti.

Mtafiti aliainisha matini kulingana na mikakati ya lugha ya urejelezi iliyotumiwa na wazee na kina mama kutokana jamii ya Abagusii na Kipsigis na mikakati ya lugha ya urejelezi iliyotumiwa na vijana kutoka jamii zote mbili. Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo.

Michoro na majedwali: Deta iliyonukuliwa imetumiwa katika kujadili hoja muhimu. Mifano ya deta hiyo ya mazungumzo iliyotumiwa katika majadiliano imewekwa kwa maandishi tofauti ambayo ni ya *Calibri* na kutiwa kwenye kisanduku. Kila mfano umepewa nambari kuanzia nambari moja na ni endelevu.

### 3.8 Maadili ya utafiti

Utafiti huu uliwatumia watu kama washiriki wa utafiti, na washiriki walipewa majana ambayo si yao halisi. Majina yalipeanwa kulingana na jamii ambayo mtafiwa anatoka. Mtafiti alitarajiwa kuzingatia maadili ya utafiti. Kwa hiyo mtafiti alitafuta idhini ya utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Egerton. Pia mtafiti alitafuta idhini kutoka kwa Tume ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi. Nyanjani, mtafiti aliwapa washiriki uhuru wa kuchagua kushiriki au kutoshiriki katika utafiti. Washiriki walihakikishiwa kuwa hakuna athari yoyote chanya au hasi ambayo ingewakumba kushiriki au kutoshiriki kwenye utafiti.

## SURA YA NNE

## UCHANGANUZI, UWASILISHAJI NA UFASIRI WA DETA

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inaagazia deta iliyokusanywa na kuchanganuliwa. Deta hii imewasilishwa kwa njia ya maelezo. Aidha sura hii iliangazia deta kwa kuzingatia malengo ya utafiti kwa kuongozwa na nadharia ya Utambulisho wa Lugha za Kikabila inayohusumakabila/mbari za binadamu na mahusiano kati ya jamii, yaani '*Ethnolinguistics identity theory*, (ELIT). Nadharia hii inabainisha na kueleza lugha ya urejelezi inayotumiwa na jamii mbalimbali ulimwenguni. Aidha inatoa mwelekeo wa kujadili athari za lugha ya urejelezi inayotumiwa na jamii ya Abagusii na Kipsigis na athari zake katika mahusiano yao. Vilevilekutathmini mbinu za suluhisho zinazotumiwa na jamii hizi kuunda uhusiano bora kati yao. Katika sehemu hii mtafiti alifasiri deta ya utafiti huu kwa kina.

### 4.2 Lugha ya Urejelezi Miongoni mwa Abagusii na Kipsigis

Jamii za Abagusii na Kipsigis zina lugha mahususi ya kurejeleana ambayo hajawai kufanyiwa utafiti. Hali hii ndio ilimfanya mtafiti kuchanganua jambo hili ili kufahamisha jamii pana kuwa pamoja na matukio mengine yanayozua vurugu, rabsha na vita vya kijamii, matumizi ya urejelezi vilevile ni miongoni mwa madhara haya.

Mfano wa isitilahi za urejelezi za kijumla ni kama vile: *bwongobwongo, korera, Omobisa, simbiri nyamoibi, omonyamato, matomasungunanu* kwa upande wa Abagusii na *nyamutio tinge, kamama, bunyo, gosobinde, bomori* upande wa Kipsigis. Isitilahi hizi hutumwa na wazee, vijana na kina mama katika shughuli zao za maisha yao ya kila siku. Kwa mfano, *kamama* ni istilahi inayotumiwa na jamii ya Kipsigis kurejelea jamii ya Abagusii inayo maanisha kuwa hawa ni watu wetu.

Hata hivyo, katika istilahi hizi kuna uzoefu wa matumizi ya istilahikati ya jamii zote mbili. *Omworo* hurejelea mwanamke ambaye hufanya kazi yake kwa uvivu na polepole sana miongoni mwa jamii ya Abagusiina hurejeleamwanamke wajamii ya Kipsigis aliyeolewa miongoni mwa jamii ya Abagusii. Kwa mfano, vijana wa Abagusii wanamfananisha na mwanamke mvivu anayefanya kazi bila haraka yoyote. Kwa hivyo kulingana na washiriki

haiwezekani kupata binti wa jamii ya Abagusii akiitwa *Omworo.*Mifano ya mahojiano ifuayo miongoni mwa jamii ya Abagusii na Kipsigis inathibitisha matumizi ya istilahi hizi.

**Mtf:** '*I want to ask you, majina hii community inawaita nawengine wanawaita*?'

**Mfanao 1:**

***1. Mzee Rchard mogaka:*** *kwa upande huu ndio nakuambia ni watu wa kunyenyekea that's why they call us nyamutio, watu wa polepole lakini wale ni wa haraka. So, you can not get a* ***Nyamutio*** *in Kipsigis*

***Mtf:*** *so nyamutio comes from this side ya Kipsigis?*

***2. Mzee Richard Mogaka:*** *ndio nyamutio ni kutoka Kipsigis*

***3. David matoke: nyamutio*** *ni mtu mpole na wanaorejelewa hapa ni Abagusii. Hawa wanaita watu wa mlima* ***tulwet.***

***(Kiambatisho: 10A 24/3/2022)***

*Omworo*, kama alivyoeleza mtafiti ni urejelezi wa jamii ya Abagusii ambapo urejelea mwanamke aliyeolewa na kijana wa Abagusii na ina maana ya mwanamkemvivu na mpole asiye na mambo mengi yaani, *Omwororo.* Kwa mktadha huu ni binti kutoka jamii ya Kipsigisasiye na kelele na wala ugomvi. Wanawake wa Kipsigis wanajulikana kwa jina hili kwani wao huwa wapole, hukwepa ugomvi hata na waume zao na huwa wakarimu. Wanapoolewa katika jamii ya Abagusii, wanaume wa Abagusii hufurahi kwa sababu wanaweza kufanya chochote wanachotaka ikiwemo kuuza ng'ombe pasi na mke wake mwenye asili ya Kipsigis kuzua vurugu au ugomvi wa aina yoyote. Matumizi ya urejelezi huu hudunisha jamii ya Abagusii na jamii hukataa matumizi haya dhidi yao (Stell & Fox, 2014)

**Mfano 2:**

***1. Mzee Joseph Arap Langat:*** *eeh anafanya kazi kama teinge sasa huyo ako na nguvu atafanya kazi yake sawasawa kwa bidii. Lakini yule wa Kipsigis utasema chorire au saa zingine nyamutio juu anafanya kazi yake polepole.*

***(Kiambatisho 10 C: 24/3/2022)***

Kwa upande mwingine mwanamke wa jamii ya Abagusii akiolewa katika jamii ya Kipsigis anarejelewa kama *teinge* yaani tingatinga kwa sababu wao hufanya kazi kwa nguvu na bidii. Pia, anaweza kurejelewa kama *bwangobwango (omwango)*miongoni mwa jamii ya Abagusiiyaani mtu anyaefanya kazi yake kwa haraka.

**Mfano 3:**

***Mtf:*** *ni wakati upi mnaitananga nyamutio?*

***1. Daniel Onchonga:*** *sasa tunawaita* ***nyamutio*** *hiyo ni kusema polepole watu wapole****ngorangora*** *pole pole*

***Mtf:*** *Ngorangora inamaanisha?*

***2. Daniel Onchonga:*** *polepole*

***3. David Obino:*** *wao wako (Abagusii)* ***bwangobwango****/harakaharaka yaani speedy.*

***Mtf:*** *sehemu ya ndoa nilisikia wakati mkipsigis ameoa Mkisiihuyo msichanaameolewa wanamwita* ***tingatinga.***

***4.Moses Gichana:*** *kwa sababu ana nguvum, Omworo ndio tunaita awa.*

***(Kiambatisho 10 C:24/03/2022)***

Lugha ya urejelezi katika jamii ya Kipsigis na Abagusii hutumika kwa kutegemea misimu na nyakati mbalimbali kama vile misimu ya ndoana wakati wa sherehe na urafiki.

### 4.2.1 Lugha Urejelezi wakati wa Uhasama kati ya Abagusii na Kipsigis

Kulingana na Hellen (2016), uhasama miongoni mwa jamii ya Abagusii na Kipsigis hutokea kwa sababu ya wizi wa mifugo na wakati wa siasa. Vijana wanaokwenda kuiba mifugo hutumia lugha rejelezi mahususi ili kutenga aliye mmoja wao na asiye mmoja wao. Istilahi yaurejelezi iliyojitokeza kwa wingi wakati wa uhasama ni *bunyo*. Ni neno lenye asili ya Kipsigis. Hutumiwa na Kipsigis kurejelea jamii ya Abagusii ili kuashiria adui yupo miongoni mwao. Pia, hutumiwa kuwarejelea Abagusii kama neno la kijumla linalomaanisha kuwa mrejelewa ni adui.

**Mfano 4:**

***Mtf:*** *sasa huku ni mpaka na mnaishi pamoja. Kuna majinaAmbayomnatumia kuitana? For example, kuna majina Mnaitanawakati wa conflicts ama inaleta kugombana?*

***1. Mzee Meto Arap Koech:*** *Huku kumekuwa na conflicts one of the reasons za conflicts ni wizi wa mifugo na siasa.*

***2. Daniel Kimosop:*** *Yaani hiyo conflict kwa sisi inatokana* ***wakati wa ng'ombe Kuibiwa.***

***3. Mzee Meto Arap Koech:*** *Unajua wherever conflicts arise, wakati conflict imeanza na usually when there is a fight it was suprising because these guys wanajua. But jina yaani matamshi ambayo ni ya hapa ni wanaita* ***bunyo kumaanisha aduithey speak that word that is our enemy*** *na* ***hiyo enemity imekaa because whoever is not a kipsigis is an enemy.***

***(Kiambatisho 10 E: 25/3/2022)***

Wazee hawa walithibitisha kuwa asili ya vurugu katika eneo hili la Borabu ni wizi wa mifugo hii inatokana na kuwawanaishi pamoja kwenye mpaka na wanaelewa matukio ya maeneo hayo. Walieza kuwa vijana ambao mara nyingi hujihusisha na vita wanajuana. Kwa hivyo neno *bunyo* linatumika miongoni mwa Kipsigis. Kauli ya Mzee wa Kipsigis kuwa; kwa Kipsigis, yeyote ambaye si Kipsigis ilithibitishwa na kauli ya vijana na hivyo alipaswa kujihathari kwa kuwa huchukuliwa kuwa adui ya Kipsigis.

**Mfano 5:**

***Mtf:*** *Nataka niulize hivi, mnafanyaje kazi huku kwa sababu mmechanganyika pamoja?*

***Moses Gichana:*** *wako kivyao. Hawa watu hawataki kukaa pamoja na wakisii. Wanataka wawe na kikundi chao.*

***Mtf:*** *hawa ni akina nani?*

***David Obino:*** *Hawa ni wakisii (akionyesha kwa kidole kikundi cha vijana walio upande wa pili) kuna wale wamesimama pale,* ***wanajitenga hawataki kuwa pamoja.***

***Moses Gichana:*** *yaani nilikuwa namaanisha, hawa mandugu zetu hawafanyi biashara kwa upamoja...* ***Kwa maneno***

***tunaongea tunasalimiana vizuri tunakuwa marafiki lakini ni watu wanajaribu kujitenga.*** *Hata ukiangalia barabara tuko wanabodaboda lakini* ***sasa unapata hawawezi kulete pikipiki zao wajumuishe kwa wengine.***

***Mtf:*** *kwa nini*

***Moses Gichana:*** *yaani mafikira yao.*

***Mtf:*** *ama mnawafukuza.*

***Moses Gichana:*** *hapana.*

***Mtf:*** *wao wamewafukuza?*

***Moses Gichana:*** *hakuna wacha nikupee mfano, angalia pale, sasa vile umeketi hivyo angalia huko, wale ni wakisii wamesimama pale lakini ile stage ni yao (Kipsigis. Wametoa pikipiki wamesongesha mbele kidogo ni ukweli wale si wa hapa lakini stage ni yao*

***Samuel Nyariki:*** *eeeh kwa sababu ile side ndio kwao Bomet*

***Moses Gichana:*** *eeeh ni yao lakini wakipata wakisii wamekuwa wawili watatu wanajitenga kwa kuwa itikadi zao na za Abagusii hazirandani.*

***(Kiambatisho 10 F:24/3/2022)***

Kauli ya vijana hawa huenda isionyeshe moja kwa moja kuwa jamii ya Kipsigis wanachukulia watu wengine wasio Kipsigis kuwa maadui, lakini inaonyesha kuwa hawana mazoea ya kutangamana na jamii jirani ya Abagusii. Jamii ya Kipsigis wanaona ni heri waache eneo lao la kazi (steji ya bodaboda) kwa sababu bodaboda za vijana wa jamii ya Abagusii zimekuja katika eneo hilo. Kwa misingi hii, inaonekana kuwa jamii ya Kipsigis inajitambua kuwa wao ni jamii tofauti na jimii nyingine na hivyo basi wanajitenga kijamii kama inavyoeleza Nadharia ya Utambulisho wa Lugha za Kikabila inayohusu makabila/mbari za binadamu na mahusiano kati ya jamii. *Bunyot* ni istilahi ya urejelezi inayotumiwa na Kipsigis kurejelea Abagusii wakati wa uhasama. Kwa upande wa Abagusii wanawarejelea Kipsigis kama *omobisa*. Hii inaonyesha wazi wazi kuwa kuna uhasama kati ya jamii hizi mbili, uhasama ambao ni fiche hasa miongoni mwa jamii ya Kipsigis.

**Mfano 6:**

***Mtf:*** *tumeambiwa kuna urejelezi bunyo*

***1.Mzee Joseph Arap Langat:*** *ni* ***Bunyot, bunyot*** *ni enemy*

***Mtf:*** *ooh ni bunyot.*

***2.Daniel Kimosop:*** *kwa upande wa kisii ni* ***omobisa.***

***3.Mzee Joseph Arap Langat:*** *tunaita hao* ***bunyot*** *wanasema* ***omobisa.***

***(Kiambatisho F:25/3/2022)***

Uhasama uliopo baina ya jamii hizi mbili majirani inasemekana ni uhasama ambao haujaanza hivi karibuni. Mzee Meto Arap Koech: kutoka jamii ya Kipsigis alieleza kuwa chanzo cha uhasama huu ni mifugo. Kuwa jamii ya Kipsigis huamini kuwa mifugo ni yao ilhali ukulima ni wa Abagusii. Ili kuonyesha jinsi uhasama huu ulianzia zamani alitamba kisasili kilichoonyesha kuwa uhasama huu ulikuwa wa zamani za kale.

**Mfano 7:**

***Mzee Meto Arap Koech:*** *unajua wherever conflicts arise, wakati conflict imeanza na usually when there is a fight it was suprising because these guys wanajua. But jina yaani matamshi ambayo ni ya hapa ni wanaita "bunyot kumaanisha adui, they speak that word that is our enemy na hiyo enemity imekaa because whoever is not a kipsigis is an enemy". "Wanaitana adui because ile uadui yenye ilianza huko Manga. You said you come from Manga, si you know that valley?"*

***Mtf:*** *"I don't know very well kwa sababu sijakulia huko, babanguAlihama maeneo yale zamani sana".*

***Mzee Meto Arap Koech:*** *When you go to Manga, Manga sub-county headquaters saahii, unatembea nchi iko flat hivi lakini inaenda kukatikaso hiyo shimo ambaye iko hapo chini ambayo hawajaishi mpaka wa leo inatunaambia kupitia historia kwamba wakipsigis walienda a very large group kwenda kuiba ng'ombe lakini kwa sababu bonde iko na gate moja, wakangojewa wote waingie kwa hiyo gate halafu Wakisii wakaitana na Wajaluo. Si unajua hiyo Marani area si mbali na wajaluo sasa wakaitana those days about 19*

*what, 18 something about 1868. So, we are told in history that hao watu waliuliwa*

***Mtf:*** *Wakipsigis?*

***Mzee Meto Arap Koech:*** *wengi wengi. Wenye walipata hata kuponyoka ni wale walikuwa wamejificha kwa chini ya maiti, wamejifunika na damu. So, when they were searching for whoever is alive tuliambiwa very few people came from there na hii ni ushirikiano ya wakisii na wajaluo,* ***wakamaliza hawa majamaa.*** *So uadui ikaanza hapo uadui because karibu all men were killed mpaka waliporudi the multiplication ya kuzaa ilianza. It was open for anybody, sasa hakuna mwenye bibi wakazaana mpaka wakapata jamii. It is understood hiyo uadui ilianzia hapo*

***Mtf:*** *ok now that is the history of uadui ya Kipsigis na Abagusii*

***Mzee Meto Arap Koech:*** *yeah, kwa sababu waliuliwa watu wengi. Kwa upande wa jamii ya Abagusii, neno linalotumiwa kuwarejelea Kipsigis wakati wa uhasama au wakati wa usiri katika mazungumzo ni omonyamato, kumaanisha mtu aliyetobolewa masikio. Jamii ya Kipisigis wana ufahamu kuwa Abagusii huwarejelea hivi na kila wanaposikia jina hilo wao hukasirika kwa kuwa kulingana na wao, urejelezi huu una maana kuwa Kipsigis ni watu ambao hawaelewi kwa urahisi.*

**Mfano 8**

***Mtf:*** *kwa maongezi yenu pengine hamtaki mtu ajue mnaongeakuhusu wakipsigis huwa mnawaitaje ama wakati wa vita?*

***1.Mary Kerubo:*** *hiyo lugha tunatumia wakati tunataka kujua mwenye yuko hapa* **Omonyamato** *atambulike kuwa ndiye huyu ili kama tulikuwa tunaongelea chochote cha siri wajue ili yeyote asiseme.*

***2. Eunice Moraa:*** *Unajua* **Omonyamato tunamaanisha kutobolewa masikio** *ili huyomtu ajue tofauti. Yaani tunamuita adui*

***3. Mary Kerubo:*** *walikuja wakakataa kuwa tukiwaita omurumbwa inamaanishambwa*

***Mtf:*** *sasa* ***omurumbwa*** *inamaanisha nini?*

***4. Mary Kerubo:*** *Mtu aliye toka sehemu inayojulikana kama Lumwa hapo zamanikidigo.*

***5. Milka Nyambaso:*** *tumesema omobisa, omurumbwa, omutumera igoro, omonyamato.*

***(kiamabatisho G:24/3/2022)***

Jamii ya kipsigis walikuwa wakitoboa masikio zamani. Katika hali ya kuvaa mapambo ile sehemu ya masikio iliyotobolewa ilifunguka na kuwa kubwa zaidi ya shimo asilia. Kadri muda ulivyokwenda, sehemu ile au ile shimo iliendelea kuwa kubwa. Kutokana na desturi hii jamii ya Abagusii wamekuwa na mazoea ya kuwaita jamii ya Kipsigis*omonyamato na Omobisa.* Miongoni mwa Abagusii, hili ni jina linalomaanisha adui yupo miongoni mwao. Pia inatumiwa wakati wa vita kati ya Abagusii na Kipsigis kuwarejelea Kipsigis kama adui. Jina *omurumbwa* pia hutumiwa na Abagusii kuwarejelea Kipsigis. Hata hivyo, jamii ya Kipsigis hawapendi jina hili na huchukulia kuwa linamaanisha mbwa. Hata hivyo maelezo ya wazee walioshiriki utafiti huu yalionyesha chanzo cha jina hili *Omurumbwa*. Ili kutoa maelezo kuhusu asili ya neno *omurumbwa,* kisasili kilitolewa na mzee kutoka jamii ya Kipsigis.

**Mfano 9:**
***Mtf:*** *kuna ingine gani mnaweza kumbuka?*

***1 Mzee Joseph Arap Langat:*** *oh, iko jambo hapo.* ***Kisii anaita sisi abarumbwa*** *na iko sababu. Iko hivi, wazungu alianzia mbali kufukuza sisi kwa upande ile.*

***Mtf:*** *Huko inaitwaje? Pande ile ni wapi huko?*

***2.Mzee Joseph Arap Langat:*** *Inaitwa Lumbwa*

***3. Mzee Joseph Arap Langat:*** *sasa alifukuza watu yetu mbele ya hapo Lumbwa mbele, akasongeza watu, akasongeza watu mpaka akafika mtoni, hapa iko mtoni Choria. Kufika hapo tukamwambia sasahapana fukuza sisi kwa sababu nyinyi hapana weza kuvuka hii mtoni na wazungu ilikuwa hivyo, kuna bunduki. Wazungu anasema tufanye nini sasa, tufanye muma(kiapo.*

***4.Daniel Kimosop:*** *tufanye kiapo, sasa hatutakuja pande hii. Tutakula kiapo.*

***5.Mzee Joseph Arap Langat:*** *Kama ni kupigana tutapigania hapo sasa, sasa wazungu nao hawakuji ng'ambo hii, sasa kitu gani tutafanya,* ***tukamate mbwa, tukate katikati kama kiapo.***

***Mtf:*** *ile mbwa ikatumika kama kiapo?*

***6. Mzee Joseph Arap Langat:*** *wakale wakakamta pande hii na wazungu pande hii, wakavuruta ikakatwa katikati sasa wazungu wakasema enda pande ile wazungu wakavuka ng'ambo ile. Wakaita hiyo jina Abarumbwa*

***7. Daniel Kimosop:*** *Kisii ndio wakaanza kuwaita hivyo.*

***8. Mzee Joseph Arap Langat:*** *Abarumbwa (Rumbwa - kutokana na jamiiya Abagusii) wamekuja huku.*

***Mtf:*** *na sasa wakisii walijuaje mbwa alikatwa kati ya Wakipsigis na Wazungu?*

***9. Mzee Joseph Arap Langat:*** *unajua tulikuwa tukipakana pamoja kutoka nchi za Mbali.*

*Mtf: Mlikuwa mkiteremka pamoja?*

***10. Mzee Joseph Arap Langat:*** *eeeh na wajaluo walikuwa katikati na Kisii iko nyuma na wajaluo inafuata sisi*

***(Kiambatisho H:24/2/2022)***

Ingawa kutokana na maelezo ya washiriki Kipsigis hawataki kuitwa *omurumbwa* na jamii ya Abagusii.Kisasili hiki kinaonyesha asili ya neno hili. Ni wazi kuwa huenda vijana hawaelewi asili ya istilahi hii na ndio maana wanapoitwa hivyo na wenzao kutoka jamii ya Abagusii wanakasirika na kuchukulia kuwa wameitwa mbwa. Mbwa ni jina lilitokana na kiapo kati ya jamii ya Kipsigis na wazungu ili kufikisha kikomo cha vita kati ya wazungu na jamii ya Kipsigis.

Katika maingilaino ya kila siku, kuna baadhi ya matumizi ya urejeleziambayo yakitumiwa kurejeleana huwa kama uchokozi na hivyo wanajamii wa Kipsigis na Abagusii wanaotangamana wakati huo hupandwa na hasira ambayo hatimaye huzua mitafaruku na vita kati yao. Urejelezi huu mara nyingi una msingi katika utamaduni wa kutahiri. Jamii ya Kipsigis na Abagusii wote hutahirisha vijana wao wa kiume wanapofika umri wa uzulufu. Istilahi za urejelezi kama vile *ngetai, ngete, omoisia* zinapotumiwa miongoni mwa vijana wa kiume,

huzua rabsha na huwa ishara ya uchokozi. Anayeitwa kwa istilahi hizi hukasirika. Miongoni mwa wanawake istilahi za urejelezi zinazozua hasira ni *egesegene* upande wa Abagusii na *chepto* upande wa Kipsigis. Hata hivyo istilahi hizi za wanawake zinaacha kutumika kutokana na marufuku ya kuwatahiri wanawake. *Ngetai, ngete* na *omoisia* ni isitilahi za Kipsigis na Abagusii mtawalia zinazotumiwa na jamii hizi kurejeleana kwa hali ya uchokozi au uhasama. Istilahi hizi zinamaanisha mtu ambaye hajatahiri ilhali katikajamii hizi mbili dhana ya mwanaume kutahiri ni kaida muhimu. Kutahiri ni mojawapo ya njia ya utambulisho kuwa kijana aliyetahiriwa amepita kiwango cha utoto na amekubalika miongoni mwa jamii kama ameingia katika kiwango cha kati miongoni mwa jamii hizi mbili kama inavyoelezewa na jamii hizi mbili za Abagusii na Kipsigis.

**Mfano 10:**

***Mtf:*** *na wakitaka kusema unajua huyu ni mtu ametahiri lakini ana utoto na utundu?*

***1.Mzee Meto Arap Koech:*** *wanita* ***Ngetai*** *ama* ***ngete***

***Mtf:*** *na hiyo ni uchokozi?*

***2.Mzee Meto Arap Koech:*** *and you know Wakisii Vijana wakitaka kuchokozana unajua mtu akiitwa omoisia hasira inapanda juu. Vijana wanajua omoisia ni kutusiwa na yule wa upande huu akiitwa ngetai au ngeta anajua amemtusi. So, that is another language ambayo inaleta shida*

***Mtf:*** *na upande wa wanawake?*

***3.Mzee Meto Arap Koech:*** *wanawake you know wanawake hawafikiani sana. Si unajua wakisii wanasema* ***egesagane*** *na upande huu wanaita* ***chepto*** *not double 'o' ni yule hajatahiri.*

***Mtf:*** *na akiitwa hivyo na hajatahiri anasikia vibaya*

***4. Mzee Meto Arap Koech:*** *yeah.*

***(Kiambatisho I:25/3/2022)***

### 4.2.2 Lugha ya Urejelezi Wakatiwa furaha

Utafiti huu ulibaini kuwa si lugha yote ya urejelezi miongoni mwa Abagusii na Kipsigis ilizua uhasama na vita. Kuna lugha mahususi ambayo wao hutumia kurejeleana wakati wa furaha. Nyakati hizi hasa za furaha kulingana na wao ni nyakati zisizo za siasa.

**Mfano 11:**

*Mtf: nawaulizaje, vile mko sahii, mko na woga, mko na furaha na wao?*

***1.MzeeMoses Rioba:*** *Sasa watu wa* ***siasa kama hawapo tuna uhusiano mwema*** *lakini siasa ikija huo uhusiano unaharibika, wanaongea pale na hapa. Unapata wale tulikuwa na uhusiano mwema tunakosana.*

***2.Mzee Nyanchoka:*** *kama saa hii* ***siasa inataka kuanza watu wa hapo wanaongea Vizuri.***

***(Kiambatisho J: 24/3/2022)***

Maelezo ya washiriki hawa ni ithibati kuwa huwa kuna nyakati ambazo majirani hawa wana uhusiano mwema na kipindi cha utulivu. Katika kipindi hiki ambacho ndichokipindi kirefu ikilinganishwa na msimu wa uhasama, istilahi maarufu ya urejelezi katika jamii zote mbili ni *kamama.* Ingawa istilahi hii ya urejelezi inatumiwa kurejeleana katika pande zote, asili yake inajikita sana katika jamii ya Kipsigis. Hivyo *kamama* kulingana na jamii ya Kipsigis wanachukulia jamii ya Abagusii kama mama yao. Kuna sehemu ya Wakipsigis hasa vijana, wanaichukulia jamii ya Abagusii kuwa mjomba. Haya yote, misingi yake imo katika jina *kamama*.

**Mfano 12:**

***1 Mzee Joseph Arap Langat:*** *and there is a good word for your research* ***kamama.*** *You see kamama ni mahali mama ametokea. We refer to these guys because nyuma* ***kulikuwa na njaa*** *na kwa sababu kulikuwa nanjaa, they exchanged wimbi na watoto. That's why in Bomet area we find a clan which is purely Kisii.*

***Mtf:*** *nani walileta watoto na nani walipeana wimbi?*

***2 Mzee Joseph Arap Langat:*** *Wakisii walipeana wimbi ndio watoto waende huko*

***3 Daniel Kimosop:**so, we call them kamama*

***4 Mzee Joseph Arap Langat:** ndio ulisikia saa zingine wakibembeleza kipsigis wanamwambia kamama kwa nini tupigane na sisi ni kamama?*

**(*Kiambatisho K:25/3/2022)***

Inabainika kuwa *kamama* ni istilahi yenye uzito, kwani hutumiwa kama chombo cha kuleta amani. Wakati wa uhasama au vita kati ya jamii hizi mbili, *kamama* hutumiwa kama istilahi shawishi ili kutuliza hali na kupunguza joto ya uhasama kama anavyoelezea mshiriki.

**Mfano 13:**

*Mtf: na wakati hii hali imetokea kati ya jamii zote mbili kwaMfano Wakipsigis wanaita Abagusii kamama, kamama inamaanisha nini?*

***1. Mzee James Kipsang:**hiyo ni long ago unajua zamani sana kulikuwa na watoto wetu, siku ya drought au kiangazi Kipsigis walikuwa na taabu, hawakukuwa na wimbi ya kuplant lakini wakisii walikuwa na hiyo knowledge. Sasa kipsigis hawakukuwa na namna ya kufanya. Walipatia wakisii watoto halafu wanawapatia wimbi. "Sasa kupitia namna hiyo wanasema kamama wakipsigis wanaona mama yao".*

***Mtf:** nani wanasema?*

***2. Mzee James Kipsang:** wakipsigis wanasema kamama kwa sababu wamewapatia mtoto halafu wanapatia chakula (wimbi)*

***3. Moses Arap Rotich:** kamama ni kumaanisha ile ishara kuleta kitu ya kupeanakwa mzazi wanalete kitu sasa wakipsigis wanaona mama yao.*

Asili ya *kamama* ni kiangazi cha zamani. Kiasilia, jamii ya Kipsigis ni wafugaji ilhali jamii ya Abagusii ni wakulima. Kwa kawaida kunapotokea kiangazi kunakuwa na uhaba wa chakula cha binadamu na mifugo. Ukosefu wa chakula cha kutosha na maji kwa wanyama huwafanya kufa. Kulipotokea kiangazi, jamii ya Kipsigis haikuwa na chakula na mifugo yao pia waliathirika. Wakati huo, kwa sababu jamiiya Abagusii walikuwa wakulima, walikuwa na chakula. Ili kuweza kuishi katika msimu huu ambapo jamii ya Kipsigis hawakuwa na chochote, jamii ya Kipsigis waliwapa Abagusii watoto wao nao jamii ya Abagusii wakawapa jamii ya Kipsigis chakula (wimbi). Ikawa kuna kubadilisha watoto kwa wimbi.

**Mfano 14:**
***1.Mzee James Kipsang:*** *kamama.... kamama wanaitana*
***2.Meshak Koech:*** *ni mjomba kwa sababu* ***sisi tulikuwa “tunapeana watoto*** *huko na wao* ***walikua wanapea sisi chakula”****, “mjomba ni hivyo tu,”*

***(Kiambatisho L: 25/3/2022)***

Matumizi ya istilahi rejelezi *kamama* iliunda msingi wa uhusiano mwema kati ya jamii ya Kipsigis na Abagusii. Uhusiano huu umeendelea mpaka sasa hivi kwamba hata kizazi cha sasa kinajua matumizi yake na wanaelewa matumizi na chanzo chake. Kulingana na vijana wa jamii ya Abagusii, istilahi rejelezi yenye urafiki ni *gosobe/gosobinde*. *Gosobe* inasemekana ni ufupisho wa *gosobinde*. Isitilahi hiihutumiwa na jamii ya Kipsigis kurejelea jamii ya Abagusii. Vijana wa Abagusii huchukulia kuwa istilahi hii inamaanisha *Mkisii* yaani anayezungumza lugha ya Abagusii.Istilahi hii miongoni mwa jamii hizi mbili ni jambo la kawaida, inayotumiwa wakati wowote bila kuzua rabsha, vurugu au vita. Ingawa *gosobe* na *gosobinde* inachukuliwa na vijana kumaanisha *Mkisii*, kuna maana nyingine ambayo inajificha katika historia. Ni maana ambayo wazee tu wanaijua ama kuielewa. Istilahi hizi zimekubalika miongoni mwa vijana na wazee ila ni wazee wanaoelewa maana kamili ya istilahi hizi. Wazee wanaeleza kuwa istilahi *gosobinde* inamaanisha mponyaji, yaani mtu wa jamii ya Abagusii aliyetibu jamii ya Kipsigis walipokuwa wanakufa kutokana na magonjwa anathibitisha kuwa Abagusii walikuwa na umilisi wa uponyaji kipindi kile. Ujio wa *gosobinde* vilevile kama *kamama* ikajenga msingi wa uhusiano mwema kati ya jamii ya Kipsigis na Ababgusii (Nyamboga, 2019). Mfano 16: Jamii ya Abagusii wanarejelewa kwa istilahi hii hawana tatizo na wameizoea.

**Mfano 15:**

***Mtf:*** *ok, that’s one part. Mnawaitaje, kuna majina ambayo mnawaita wakati mnatekeleza kazi zenu?*

***1. Mzee Omwamba Isanda:*** *wao wanatuita gosobe na sisi tunawaita wakale.*

***Mtf:*** *ati mnawaitaje?*

***2. Mzee Omwamba Isanda:*** *gosobe*

***3.Mzee Nyanchoka:*** *wakale ndio wanatuita gosobe*

***4.Mzee Moses Rioba:*** *ingine wanatumia wakati wanakuzungumzia kisiri wamezoea Kusema gosobe*

*Mtf: gosobe, bosobe, gosobindelina maana gani?*

***5.Mzee Moses Rioba:*** *Gosobinde kwa Kikipsigis tunaweza waita wakisii*

***6.Mzee Nyanchoka:*** *Gosobe ni shortcut ya gosobinde*

***Mtf:*** *sasa nataka nijue ile majina mnaita wakipsigis ni majina gani? Kuna kama nyamotio, kama hizo hizo*

***7.Mzee Nyanchoka:*** *eeeeh kuna majina kwa mfano gosobinde. Sasa hata watoto wetu hata huyu hajui gosobinde ni nini wanajua gosobinde ni mkisii. Gosobinde ni mponyaji.*

***8.Mzee Moses Rioba:*** *Unajua kazi ya gosobinde walikuwa wanasema gosobinde kwa sababu walikuwa wanaenda saa ile watu wamekufa hapa kwa njia wanaenda kuleta miili wengine wakapone. Mkisii anaitwa gosobinde kwa maana ameponya watu hapa sasa hiyo jina ikaendelea gosobinde*

***Mtf:*** *wakati kuna sherehe je?*

***9.Antony Kibagendi:*** *Omoyega kumaanisha sherehe*

***(Kiambatisho M:25/03/2022)***

*Omoyega* ni istilahi inayomaanisha sherehe na furaha na hutumiwa katika kipindi chochote kile cha msimu wa furaha na misimu ya sherehe mbalimbali kama vile harusi, kutoa vijana jandoni na sherehe zozote zile za furaha. Ni istilahi rejelezi inayotumiwa na jamii zote mbili.

Ingawa wizi wa ng'ombe na siasa ulizua uhasama kati ya jamii ya Kipsigis na Abagusii kama majirani, historia kupitia maelezo ya visasili kutoka kwa washiriki wa utafiti unaonyesha kuwa msingi wa jamii hizi si uhasama. Visaasili walizotoa washiriki vinaonyesha kuwa msingi wa uhusiano na maingiliano kati ya jamii hizi mbili ni urafiki na ushirikiano mkubwa wakati wa dhiki. Msingi wa uhusiano, ushirikiano na maingiliano kati ya jamii hizi mbili ni ule wa akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.

### 4.2.3 Lugha ya Urejelezi Wakati wa Ndoa

Jamii ya Kipsigis na Abagusii ni majirani wanaoishi kwa pamoja na kutumia rasilimali mbalimbali kama vile barabara, maeneo ya biashara, shule za msingi na upili. Kando na hayo

wao hujumuika pamoja sokoni, katika maduka na mikahawa katika mtaa wa Chebilat. Kwa sababu ya maingiliano haya, kumekuwepo na utangamano katika kiwango cha ndoa. Istilahi za urejelezi wakati huu ni kama vile *Batiep*na *Bomori, Ahule*ambazo hutumiwa na jamii ya Kipsigis kuwarejeela Abagusiiilhali *Korera* hutumiwa na jamii ya Abagusii kurejelea jamii ya Kipsigis. Hizi ni istilahi zinazotumiwa na wazee ambao watoto wao wanaoana na hudumu maishani mwao yote kwani ndoa haina mipaka ama hata iwe waki wa siasa ama wakati jamii ziko kwenye harakati za kutoelewana.

**Mfano 17:**
***Mtf:*** *sasa apart from that, wakati wa ndoa kuna majina mnaitana?*

***1. Mzee Meto Arap Koech: Batieb*** *ni ya upande huu na upande wa**wakisii ni korera. Batieb ni mahali wamechukua msichana ya mzee Kipsigis.** Kama ameenda Kisii ama ujaluoni wanaita **Batieb kwa mama**na **mzee wanaita Bomori.**Bomori they take it as a name but iko na maana kubwa kwa sababu you see if your son married my daughter kwa mfano huyu ni bibi yako, huyuananiitaBatieb lakini mimi nakuita Bomorikama*

***2.*** *mzee, lakini mama ni Batieb*

***Mtf:*** *hiyo ni moja hakuna majina mengine isipokuwa hiyo?*

***3 Mzee Meto Arap Koech:*** *you know kama mama ametoka upande ya kisii kwa upande huu wanaita **Ahule** tuseme kama in-laws wa upande huu, so tunaita Ahule mahali mama ametoka*

***(Kiambatisho N:25/3/2022)***

**Mfano 18:**

***Mtf:*** *nyingine*

***1. Ruth Koech: Batieb,*** *korera halafu **bomori***

***Mtf:*** *Bomori ni nani?*

**2.** ***Ruth Koech: Bomori*** *ni mzee na mimi naitwa **Batieb***

Iwapo mwanaume wa Abagusii anaoa msichana wa jamii ya Kipisigis, babake huyo msichana atarejelewa kama *Bomori*na wale wa jamii ya Abagusii, ilhali mamake binti wa Kipsigis ataitwa *Batiem*Istilahi hizi zinatumiwa na jamii hizi mbili kurejeleana hadi zimekuwa mazoea hivi kwamba ni vigumu kujua iwapo asili ya istilahi hizi ni lugha ya Abagusii au Kipsigis. Jamii ya Kipsigis wanamwita mama wa binti ya Abagusii aliyeolewa miongoni mwa Kipsigis *Ahbule (Abule ikiwa na maana ya Mjomba).*

**4.2.4Lugha ya Urejelezi Miongoni mwa Marafiki**

Urafiki miongoni mwa jamii ya Abagusii na Kipsigis ina misingi yake katika maelezo ya visaasili. Hivyo wamekuwa na mahusiano ya urafiki kwa muda mrefu. Istilahi kama vile *Bomori* hutumiwa miongoni mwa wazee. *Bomori* hutumiwa miongoni mwa wazee ambao watoto wao wameoana. Hata hivyo, linatumiwa vilevile miongoni mwa wazee wa jamii ya Kipsigis na Abagusii ambao ni marafiki kurejeleana.

**Mfano 19:**

***Mtf:*** *na wazee ambao ni marafiki?*

***1.Mzee Meto Arap Koech:*** *hiyo you know when this word applies, ya marriage mtu wa heshima ni* ***Bomori*** *hata kama watoto hawajaoana mnaanza kupendana*

***Mtf:*** *nyingine*

***2.Mzee Meto Arap Koech: abasani,*** *marafiki*

***Mtf:*** *marafiki ni Kiswahili.*

***3.Mzee Meto Arap Koech:*** *ama* ***ahule, kamama,*** *hawa ni watu wamoja.*

***4.William Langat:*** *kamama usually covers a wide range.*

***(Kiambatisho O:24/3/2022)***

Majina mengine ya urafiki hasa miongoni mwa vijana ni *omosani*ni urejelezi unaomaanisha rafikina *minto* inamaanisha mtu wetu, *omwabo ni* ndugu yangu nahutumiwana vijana wa jamii ya Abagusii kurejelea wenzao kutoka jamii ya Kipsigis, *kamama* ni mjomba, *gosebinde* ni mtu kutoka jamii ya Abagusii, *nyamuti*oni mtu wetu kutoka jamii ya Abagusii.

### 4.3 Athari za Lugha ya Urejelezi katika Mahusiano ya Jamii ya Abagusii na Kipsigis

Sehemu hii inaangazia athari za lugha rejelezi inayotumiwa na jamii ya Abagusii kuwarejelea wanajamii wa Kipsigis na vilevile athari za lugha rejelezi inayotumiwa na Kipsigis kuwarejelea wanajamii waAbagusii.Matumizi ya lugha yoyote ile huwa na athari na matokeo mbalimbali kwa watumiaji. Katika muktadha huu, kwa misingi ya urejelezi inayotumiwa na jamii za Abagusii na Kipsigis, kuna athari kwa watumiaji. Ingawa urejelezi ni dhana ya kawaida hasa katika nyakati za siasa nchini Kenya. Athari za matumizi ya urejelezi huu ni chanya au hasi. Athari chanya zinaushirikiano na mwingiliano wa jamii wakati wa matumizi yake na uzua amani miongoni mwa jamii hizi. Ilhali athari hasi zina matokeo ya rabsha, vurugu na vita kati ya jamii nyingine. Sehemu hii inaangazia athari za lugha inayotumiwa na jamii ya Abagusii kuwarejelea wanajamii wa Kipsigis na vilevile athari za urejelezi unayotumiwa na Kipsigis kuwarejelea wanajamii wa Abagusii.

#### 4.3.1 Athari Hasi za Lugha ya Urejeleziambapo kuna dhana ya 'sisi; na 'wao'

Urejelezi huzua dhana ya 'sisi" na "wao" kulingana na Smirnova na Iliev (2017) na Giles na Johnson (1987). Hivyo sisi, huchukuliwa kuwa ndio watu wa ndani wa kikundi fulani ilhali wao huwa watu wa nje wa kikundi husika. Katika muktadha huu, kila wanajamii wa Abagusii walipowarejelea watu wa Kipsigis, walijirejeleana kama "sisi" ilhali watu wa jamii ya Kipsigis waliwarejelea kama "wao". Uanishaji huu ulizua tofauti kubwa na kuweka tofauti hiyo kuwa wazi. Tofauti hizi kulingana na washiriki wa utafiti huu ndio ulisababisha athari hasi kama inavyojitokeza katika mfano ufuatao:

**Mfano 20:**

***1.Moses Gichana:*** *Hawa ni wakisii, wale wamesimama pale wanajitenga hawataki kuwa pamoja na sisi.*

***2.David Obino:*** *Yaani nilikuwa namaanisha,* ***hawa mandugu zetu hawafanyi biashara kwa upamoja****, hawa ni watu wanapenda sana kujipenda, yes. Kwa maneno tunaongea tunasalimiana vizuri tunakuwa marafiki lakini ni watu ambao wanajaribu kujitenga.* ***Hata ukiangalia*** *kwa hii barabara tuko na bodaboda, sector ya bodaboda lakini sasa unapata hawawezi kuleta pikipiki zao wajumuishe na wengine*

***Mtf:*** *kwa nini?*

***4.Moses Gichana:*** *yaani mafikiria yao...*

***Mtf:*** *ama nyinyi mnafukuza hao?*

***5.Moses Gichana:*** *hapana*

***Mtf:*** *wao wanafukuza nyinyi?*

***5.Moses Gichana:*** *hapana. Wacha nikupee mfano, angalia pale, sasa vile umeketi hivyo angalia huko, wale ni Wakisii wamesimama pale, lakini ile stage ni yao, wametoa pikipiki tena wamesongesha mbele kidogo, ni ukweli hawa si wa hapa lakini stage ni yao*

***Mtf:*** *eeeh juu ile side ndio kwao Bomet*

***6.Moses Gichana: eeeh ni yao lakini wakipata wakisii wamekuwa wawili au watatu, wanajitenga****, yaani si eti wamefukuzwa au ugomvi kati yetu nao, yaani minds yao hatuelewi.*

***(Kiambatisho P:25/3/2022)***

Katika mfano 20, maelezo ya washiriki yanaonyesha kuwa kijuujuu kuna uhusiano na utangamano mzuri kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis. Hili linadhihirika pale mshiriki anaposema, “kwa maneno tunaongea tunasalimiana vizuri nakuwa marafiki”. Hata hivyo maelezo zaidi yanaonyesha kuwa kindani kuna uhasama wa aina fulani. Maelezo hapa yanaonyesha kigezo cha sisi na wao (Tajfel, 1970). Wao hapa wakiwa watu wa jamii ya Kipsigis ambao kila wanapojipata karibu na watu wa jamii ya Abagusii wanajitenga. Wako radhi hata kuwacha eneo ambalo kwa kawaida ni lao hasa katika biashara ili kujitenga na watu wa jamii ya Abagusii. Hali hii ya kujitenga katika maeneno ya kazi, biashara na hata kula yanaonyesha uhasama nyamavu, ambao hauwezi kuonekana na kujulikana na mtu wa nje isipokuwa watu wanaoishi katika jamii hizi mbili. Kando na kule kujitenga kwa jamii hizi mbili wakati wa maingiliano ya kila siku, wakati mwingine, maneno ya urejelezi yanaweza kusababisha vita kama inavyoelezwa katika mfano 21.

**Mfano 21:**

***Mtf:*** *Sasa nataka mniambie, majina gani mnajua wanawaita?*

***1.Moses Gichana:*** *Ya matusi?*

***2.Antony Kibagendi:*** *yale ya matusi au yoyote?*

***3.Antony Kibagendi:*** *Unajua yale ya kutusi ndio huleta vita, vita hazitokei kwa sababu ya kitu kubwa, ni kitu kidogo, unahisi vibaya amemtusi mkisii mwenzako, ama inawezekana wakutusi weweuhisi vibaya, mnashikilia hapo kidogo shida imeanza.*

***(Kiambatisho Q:25/3/2022)***

Maelezo ya washiriki katika mfano 21 yanaonyesha wazi kuwa kuna baadhi ya maneno ya urejelezi yanayotumiwa miongoni mwa jamii hizi mbili ambayo yana athari hasi. Athari hasi katika muktadha huu ni rabsha, vurugu, mitafaruku na vita. Mshiriki ambaye ni kijana kutoka jamii ya Abagusii anaeleza kuwa vita na mitafaruku kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis huwa haisababishwi na mambo makubwamakubwa bali ni mambo madogo kama istilahi rejelezi ambazo zitachukuliwa kuwa ni matusi na wazungumzaji. Katika hali hii, istilahi inayorejelewa na mtu mmoja inaweza kuzua vita kati ya watu wa jamii tofauti. Vita hivi vinakuwa kwa misingi ya 'mwenzetu' ama 'mtu wetu' ametukanwa. Haya yanajitokeza vizuri mshiriki anaposema kuwa 'ni kitu kidogo unahisi vibaya kuwa amemtusi Mkisii mwenzako' na hivyo kuzua mitafaruku rabsha na vita miongoni mwa jamii.

Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa istilahi ambayo itakuwa imetumiwa huenda ikazua vita kwa sababu binadamu mwingine ambaye ni mwenzako ametukanwa. Kwa misingi hii ni wazi kuwa 'Mkisii mwenzako'. Yaani 'sisi' ambao hapa ni Abagusii tumechokozwa na 'wao' ambao hapa ni Kipsigis. Ugomvi unawacha kuwa kati ya mtu na mwingine na kuwa kati ya jamii moja dhidi ya jamii nyingine, kama nadharia ya utambulisho wa lugha za kikabila inayohusu makabila/mbariza binadamu na mahusiano kati ya jamii inavyoangazia. Hivyo kuzua kuwekwa wazi uhusiano wa kitambulisho wa kiuainishi, ambapo ilimuradi yule anayechukuliwa kuwa wa kikundi fulani anachokozwa basi kundi zima huwa limechokozwa. Dhana kuwa 'mkisii mwenzako' ndiyo inayojikitokeza badala ya binadamu mwenzangu.

**Mfano 22:**

***1.Moses Gichana:*** *actually, kwa maneno ambayo ndugu hawa wenzetu wanatumiani mawili*

*2.Antony Kibagendi: Ongea kwa Kiswahili sasa*

***3. Antony Kibagendi:*** *kwa majina mabayo wanatumia ni mbili, moja ni gosobinde na nyingine ni gosobe, hiyo ndio majina wanapenda sana kutumia lakini sisi wenyewe hatujawai jua ni matusi lakini sisi tumeyazoea kwa sababu tunafikiria wanatuita jina mkisii.*

***(Kiambatisho R: 25/3/2022)***

Katika mfano 22, vijana wa jamii ya Abagusii wanaainisha majina ya urejelezi ambayo wanajua jamii ya Kipsigis hutumia kuwarejelea. Hata hivyo majina haya kufikia wakati huu hayajazua msisimko wowote miongoni mwa vijana hawa kwa sababu kama anavyoeleza kijana kutoka jamii ya Abagusii wanadhani kwamba*gosobinde* na *gosobe* si matusi. Namna anavyotoa maelezo haya pia yanaonyesha kuwa iwapo wanaweza kuthibitisha siku moja kuwa majina haya ya urejelezi ni matusi au yamebeba maana hasi basi huenda pakawepo na ugomvi kati yao na jamii ya Kipsigis ambao ndio watumizi wa istilahi hizi.

**Mfano 23:**

***Mtf:*** *sasa wakati mnasherehekea si mnaambiana tukunywe pombe ana tukule nyama choma ama mbuzi ama kitu kama hiyo?*

***1.Moses Gichana:*** *oookay, ndugu yangu nataka uelewe hawa watu hawaigii kwa pande za wakisii, hiyo sahau*

***Mtf:*** *nyinyi mnaingia kwao?*

***2.moses Gichana: wanajitenga***

***3.Antony Kibagendi:*** *lakini wewe huoni pale kwenye tunakunywa chai*

***4.Moses Gichana: wanajitenga***

***5.Antony Kibagendi:*** *hawa wanakuja wanakaa kwa hii meza na wale kwa ile lakini wanapiga stori*

***6.Moses Gichana:*** *utoke huko kwa mfano huyu vile amekaa hivi wacha niende nikae na yeye, utapata wote wametoka wametuacha na yule tulikuwa tunaongea na yeye.*

***(Kiambatisho S: 25/3/2022)***

Ni muhimu kutaja kuwa, kuna uhusiano na mlahaka mwema kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis wakati kuna utulivu miongoni mwao. Hili linaonekana katika mji huu wa Chebilat-Borabu ambapo deta ya utafiti huu ilikusanywa. Jamii zote mbili zinaoyesha dalili ya utulifu na hamna uhasama wa aina yoyote katika shughuli zao za kila siku, lakini ghafla vurugu, ghasia na vita huzuka kati ya jamii hizi majirani. Mtafiti aligundua kuwa katika maeneo ya burudani kama baa na maakuli kama hoteli jamii hizi mbili zilitangamana japo kwa tahadhari. Wateja wa kutoka jamii ya Abagusii walikaa upande mmoja ilhali wale wa kutoka jamii ya Kipsigis pia walikaa upande mwingine. Ni kama wanajamii hawa wamekwishazoea hali hii. Kando na mtafiti kushuhudia haya, maelezo ya vijana walioshirikishwa kwenye utafiti yalithibitisha haya yaliyoshuhudiwa na mtafiti. Kule kujitenga kunaonyesha kuna tofauti za kindani mno ambazo huenda zisizungumziwe waziwazi, lakini yanaongoza mahusiano na utangamano wa jamii hizi mbili. Mazungumzo ya mfano 24, yanathibitisha kuwa kuna sababu za kindani zaidi zinazozuia utangamano huru kati ya Abagusii na Kipsigis.

**Mfano 24**

***1.David Obino:*** *Jambo lingine mimi nilelewa kwa wakale almost 1976, kule mtoto akizaliwa motto anaanza kufundishwa mambo ya ukabila. Hiyo lazima enyewe meuelewe kuna ile njia mtoto anaambiwa gosobe, yaani mkisii kwa mfano tupange saii twende kwa boma ya mtu, watoto waskie gosobe, huyo mtoto hawezi kuja karibu na wewe sasa sielewe hapo.*

***Mtf:*** *sasa labda ni uadui ama ni nini?*

***2.Moses Gichana:*** *Saii mwende mpaka kwa wakale pale, utamke wewe ni mkisii, hawawezi kuja hata wakusalimie.*

***(Kiambatisho T: 25/3/2022*****)**

Mshiriki kutoka jamii ya Abagusii anaeleza kuwa amelelewa na watu wa jamii ya Kipsigis na hivyo anaelewa mienendo yao. Kwa misingi ya maelezo yake, anajaribu kuthibitisha kuwa

wanajamii wa Kipsigis wanafunzwa utambulisho wao kikabila wakiwa bado watoto. Hivyo wanapokuwa watu wazima wanajua tofauti yao na jamii ya Abagusii. Wanajua tofauti kati yao kama jamii moja na jamii ya *gosobe*. Anaeleza kuwa utambulisho huu unatambuliwa hata na watoto wadogo. Maelezo ya mshiriki huyu yanaweza kuchukuliwa kuwa madai tu. Hata hivyo, wakati wa utafiti, mtafiti aligundua kuwa mshiriki huyu alikuwa na utambulisho mara mbili: alikuwa na umilisi wa kuzungumza lugha ya Abagusi na Kipsigis. Anapotangamana na watu wa Abagusii alizungumza lugha hiyo na hivyo wakamchukulia kama mmoja wao. Kwa sababu anaelewa mtindo wa maisha, si rahisi kubaini kuwa si mmoja wao kamwe. Pia ana uwezo wa kuzungumza lugha ya Kipsigis. Anapotangamana na watu wa Kipsigis wanamchukulia kama mmoja wao. Anaelewa mienendo na mtindo wa maisha ya jamii ya Kipsigis na hivyo anajua kuishi na kutangamana kama wao na vilevile kuzungumza kama wao. Mshiriki huyu ni kama ndumakuwili kwa kuwa anauwezo wa kuchochea pande zote mbili katika eneo hili. Jamii zote mbili zimemkubali kwa sababu ana malezi ya jamii zote mbili.

Athari nyingine hasi ya urejelezi inahusiana na matumizi ya pamoja ya rasilimali. Maelezo ya vijana wa jamii ya Abagusii yanaonyesha kuwa kutokana na mahusiano mabaya ya hapo awali hasa ghasia za uchaguzi wa miaka ya 2007-2008, watu wa jamii ya Kipsigis hawapendelei kutumia shule kwa pamoja. Ingawa kuna shule ya msingi ya Nyagachu karibu na watu wengi wa jamii ya Kipsigis, hakuna mtoto yeyote wa jamii hiyo anayehudhuria shule hiyo. Hii ni kwa sababu shule hii ipo karibu nao, ila iko kwa upande wa Abagusii. Ikumbukwe kuwa jamii hizi mbili Abagusii na Kipsigis wanatenganishwa tu na barabara hivi kwamba upande mmoja ni Kaunti ya Nyamira na Kaunti ya Bomet upande.

Hivyo wanajamii wa Kipsigis wanaonelea ni bora watoto wao kutembea masafa marefu kuhudhuria shule ambayo inapatikana upande wa Bomet ilimuradi tu wasihudhurie shule iliyoko upande wa Nyamira. Kwa upande mwingine, jamii ya Abagusii wanahudhuria shule iliyoko upande wa Kipsigis na ni karibu na wao. Kwa hivyo ni jambo la kawaida kuwapata watoto wa jamii ya Abagusii katika shule ya msingi ya Nyagachu ilhali huwezi kupata mtoto yeyote wa Kipsigis katika shule ya Mogoitambu.

**Mfano 25:**

***1.Mzee Meto Arap Koech:*** *Wanaita ngetai ama ngete*

***2.Mzee koech Joseph:*** *na hiyo ni uchokozi, sawa*

***3.Mzee Meto Arap Koech:*** *and you know, wakisii vijana hapo wakitaka kuchokozana unajua mtu akiitwa omoisia, hasira inapanda juu. You know the boys who are here kwa buildings za wakisii, vijana wanajua omoisia ni kutusiwa na ule wa upande huu akiitwa ngetai au ngeta anajua amemtusi. So that is another language ambayo inaleta shida*

***Mtf:*** *Sasa niambie, hiyo ni upande wa wanaume na upande wa wanawake?*

***4.Mzee Meto Arap Koech:*** *wanawake, you know wanawake hawafikiani sana, si unajua wakisii wanasema egesagane na upande huu wanaita chepto not double 'o' ni yule hajatairi*

***5.Mzee Rotich:*** *na akiitwa hivyo na hajatairi anaskia mbaya*

***6.Mzee Meto Arap Koech:*** *yeah, so those things 2007 wakipigana kwa mpaka you know you were there, sasa wakiitwa abaisiaba wanacheka*

**7.*Mzee Daniel Kimosop:*** *wanagoroka (kicheko)*

***8.Mzee Meto Arap Koech:*** *unajua the boys here wanajua lugha zote akiona yule ni Kipsigis na yule ni mkisii anaeza kukuita ngetae sasa kwa sababu anajua meaning. So quarelling inaanza hapo.*

***(Kiambatisho U:24/3/3022)***

Katika mfano 26, kuna baadhi ya maneno za Ekegusii (Abagusii) na Kipsigis yanayojulikana na jamii zote mbili kuwa yanapotumika huamsha hasira na kuzua mizozo. Jamii ya Abagusii na Kipsigis wana utamduni wa kutahiri watoto wao wanapobalehe, hasa watoto wa kiume. Kwa hivyo, mtu mzima, mwanaume, ambaye hajatahiri huchukuliwa kuwa na kasoro. Majina ya mtu ambaye hajatahiri yanapotumiwa kurejelea mwanamume wa Abagusii na Kipsigis ambaye ametahiri huzua mizozo. Kwa mfano kama inavyoelezewa na washiriki, iwapo wanajamii wa Abagusii watarejelea mwanaume wa Kipsigis kwa kumuita *ngetai* au *ngeta* basi hiyo itakuwa

chanzo cha vita. Kufanya hivi inachukuliwa uchokozi na hivyo haichukuliwi kama mzaha. Hii ni kwa sababu wanajamii wa Kipsigis wanathamini sana utamaduni wao wa kutahiri. Upande wa Abagusii pia ni vivyo hivyo. Wanajamii wa Kipsigis pia wanapomrejelea mwanaume wa Abagusii kwa kumuita urejelezi *Omoisia,* ni uchokozi. Hiihuzua mizozo na kuwakasirisha sana watu wa Abagusii. Wanajamii hawa wote wanajua kuwa istilahi hizizina mipaka kimatumizi.

Hali hii pia ni sawa miongoni mwa wanawake. Wakati ule ambao utamaduni wa kutahiri wanawake ulipokuwa, kumuita mwanamke wa Kipsigis *chepto* inaweza kuzua vita mingoni mwa wanawake wa Kipsigis. Hali hiyo ni sawia na wanajamii wa Abagusii. Kumuita mwanamke wa Abagusii *egesagane* itazua mizozo. Kwa sababu neno hili linamaanisha mwanamke ambaye hajatahiriwa na jamii humchukulia kama mtoto ambaye hana usemi miongoni mwa wanajamii.

**Mfano 26**

***1.Mzee Meto Arap Koech:****so, kuna jambo ambayo wakisii wakitaka mkale aharibikekichwa kabisa anaitwa omonyamato. Unajua huyo ni* ***mtuametobolewa maskio, hiyo ndio watu hawataki.***

***2.Daniel Kimosop:*** *so hiyo inacause shida kabisa.*

***3.Mzee Meto Arap Koech:*** *normally kuna baraza na wazee wakiskia mkisii amesema hapo chini omonyamato anaharibika, hiyo ni uchokozi.*

***(KiambatishoV: 24/3/2022)***

Jina *omonyamato* miongoni mwa Kipsigis inamaanisha mtu ambaye ametobolewa masikio. Hapo zamani mojawapo ya tamaduni ya Kipsigis ilikuwa kutobolewa masikio. Kwa sasa ni utamaduni ambao umezikwa katika kaburi la sahau. Leo hii iwapo wanajamii wa Abagusii watatumia istilahi hii kuwarejelea wanajamii wa Kipsigis, basi huzua vita na migogoro. Wanajamii wa Kipsigis hawataki kusikia wanarejelewa hivyo kabisa. Mshiriki kutoka jamii ya Abagusii anapotumia urejelezi huu "mkale kuharibika kichwa" anamaanisha mwanajamii wa Kipisigis kukasirika na kupandwa na hasira kupita kiasi.

Kutokana na ithibati zilizotolewa, ni wazi kuwa matumizi ya lugha rejelezi ina athari hasi katika jamii hizi mbili zinazopakana na wakati huo huo ni majirani wanaotumia rasilimali

kadhaa kwa pamoja. Ni muhimu kutaja kuwa, washiriki kutoka upande wa Abagusii walikuwa na mengi ya kusema ili kuonyesha athari hizi. Hata hivyo, vijana wa jamii ya Kipsigis hawakuwa na chochote cha kusema na hii ilisababisha mtafitis kutopata deta aliyokusudia kupata hasa miongoni mwa jamii ya Kipsigis. Hata hivyo mtafiti alipata deta kutoka kwa vijana wachache kutoka jamii hii waliokubali kushiriki katika utafiti. Hili huenda lilichangiwa na ukweli kuwa mtafiti vilevile ni wa jamii ya Abagusii. Kwa sababu mtafiti alikuwa wa jamii ya Abagusii, huenda washiriki kutoka jamii ya Kipsigis walihisi kuwa mtafiti alikuwa si wa kwao na hivyo hawakuona haja ya kutoa habari muhimu alizohitaji mtafiti.

### 4.3.2 Athari Chanya za Lugha ya Urejelezi

Lugha ya urejelezi inaweza kuwa na athari chanya vilevile. Kando na kusababisha mizozo inaweza kuwafanya wazungumzaji na warejelewa kuingia katika vita vikali kutokana na athari hasi. Hata hivyo si wakati wote ambapo lugha ya urejelezi husababisha mambo mabaya. Lugha ya urejelezi inaweza kuzua mambo mazuri miongoni mwa wanaotumia lugha hiyo. Lugha ya urejelezi inaweza kuimarisha uhusiano wa wanajamii kwa njia nzuri na hivyo kutumiwa kujenga uhusiano bora miongoni mwa wanajamii (Jabbar & Hassan, 2018; Jacobson, 2006; Wright, 1997). Uhusiano mzuri ni pamoja na bishara bora, kushiriki sherehe, kuomboleza na kushiri matanga kati yao, ndoa kati yao, matumizi ya raslimali kati ya jamii hizi na kadhalika. Katika mfano 28 unaofuata, Wazee wa jamii ya Kipsigis wanaelezea majina ya urejeleo ambayo kwa muda mrefu sana yametumiwa na Abagusii na Kipsigis kuimarisha uhusiano bora kati yao.

**Mfano 27:**
***1.Mzee Joseph Arap Langat:*** *and there is a good word for your research, Kamama. Yousee kamama ni mahali mama ametoka. We refer to this guy because nyuma kulikuwa na njaa na kwa sababu kulikuwa na njaa, they exchanged wimbi na watoto. That’s why in Bometarea we find a clan which is purely Kisii*

***Mft:*** *Nani walileta watoto na nani walipeana wimbi?*

***2.Mzee Meto Arap Koech:*** *Wakisii walipeana wimbi ndio watoto waende huko*

***3.MZee kimosop:****so, we call them Kamama*

***4.Mzee Meto Arap Koech:*** *ndio ulisikia saa zingine wakibembeleza Kipsigiswanamwambia Kamama kwa nini tupigane na sisi ni Kamama.*

***(Kiambatisho W:24/3/2022)***

Wanajamii wa Kipsigis na Abagusii huitana *kamama*. Ni jina ambalo limetumiwa kwa muda mrefu sana na wanajamii hawa. Istilahi hii ina historia ndefu sana. Inatokana na msimu wa njaa katika enzi za zamani. Ili kukabiliana na njaa wakati huo, wanajamii wa Kipsigis waliomba chakula kutoka kwa Abagusii. Nao baadhi ya watoto wa Kipsigis wakapeanwa kwa Abagusii. Ikawa ni hali ya kubadilishana watoto kwa chakula. Kwa sababu hii, kulingana na washiriki kuna jamii ya Kipsigis wengi Nyamira, miongoni mwa Abagusii. Sawa na maelezo kuwa kuna wanajamii wa Abagusii wengi wanaopatikana Bomet, miongoni mwa Kipsigis. Kulingana na maelezo ya washiriki, panapotokea vurugu kati ya Kipsigis na Abagusii, mara nyingi vita hivyo hukomeshwa kwa kukumbushana historia na matumizi ya istilahi *kamama*. Matumizi haya huwa ni istilahi inayojaribukudokeza kuwa wao ni jamaa na hivyo hakuna haja ya kupigana.

**Mfano 28:**

***Mft:*** *Sasa nataka nijue ile majina mnaita wakisii ambayo iko nasiri*

***1.Mzee Joseph Arap Langat:*** *eeeeh, kuna majina tunaitana. Kwa mfano gosobinde. Sasa hata watoto wetu hata huyu hajui gosobinde ni nini.*

*Wanajua gosobindeni mkisii. Gosobinde ni mponyaji.*

***2. Mzee James Kipsang:*** *unajua kazi ya gosobinde walikuwa wanasema gosobinde kwa sababu walikuwa wanaenda saa ile watu wamekufa hapa kwa njia, wanaenda kuleta miili wengine wapone, mkisii anaitwa gosobinde kwa maana ameponya watu hapa sasa hiyo jina ikaendelea gosobinde.*

***(Kambatisho X: 24/3/2023)***

Kulingana na mshiriki kutoka jamii ya Kipsigis, hata watoto wa kisasa hawajui maana ya *gosobinde.* Hata hivyo *gosobinde* ni neno ambalo lina historia ndefu na lenye kuonyesha asili

ya uhusiano mwema kati ya Kipsigis na Abagusii. Wazee hawa wanasema kuwa jina hili lilitokana na hali ya Abagusii kuwasaidia kwa kuwatibu walipokuwa wanakumbwa na magonjwa. Kulingana na (Sindiga, 1995). Abagusii walikuwa waganga waponyaji ambao walitoa huduma za uponyaji kwa Abagusii na Kipsigis. Wanajamii wa Kipsigis walipouwawa katika vita na jamii zingine, Abagusii wangeenda kuchukua miili yao na kuwasaidia wale ambao walikuwa wameumizwa vibaya. Kuanzia wakati huo, kumekuwa na uhusiano mwema, kwa sababu Abagusii ni waponyaji wao (Asare-Danso, 2005; Sindiga, 1995).

## 4.4. Mbinu za Suluhisho Zinazotumiwa na Abagusii na Kipsigis Kuimarisha Uhusiano Mwema kati yao

Migogoro na hata vita kutokana na lugha ya urejelezi ni jambo la kawaida miongoni mwa wanajamii na watu wenye mahusiano mbalimbali kote ulimwenguni, Afrika na hata Kenya. Kila kundi la watu lina njia yao wenyewe ya kukabiliana na migogoro na kutatua mizozo kati ya wanajamii (Ajayi & Buhari, 2014). Wanaongezea kuwa jamii mbalimbali za Afrika wana njia anuwai za kusuluhisha mizozo kati ya wanajamii wao. Wanaelezea kupitia mfano wa jamii ya Yoruba ambayo walitumia chifu (*Ile-ejo ijoye Adugbo),* Mfalme (*Ile-ejo Oba)* na kikao cha machifu (*Igbimo Ilu)* kusuluhisha mizozo kati ya wanajamii. Katika sehemu hii, kazi hii iliangazia mbinu ambazo wanajamii wa Abagusii na Kipsigis wanatumia kuimarisha uhusiano wao kama majirani wanaoishi katika eneo moja ili kuimarisha maendeleo, kuendeleza ujirani mwema na kujenga amani. Ikumbukwe kuwa utafiti huu uliangazia lugha ya urejelezi iliyotumiwa na washiriki hivyo mbinu za suluhisho ziliainishwa kutoka kwa mazungumzo ya washiriki. Kutokana na mazungumzo kati ya mtafiti na washiriki, ilibainika kuwa migogoro kati ya Abagusii na Kipsigis ilikomeshwa na uwepo wa ndoa za mseto kati ya wanajamii kutoka jamii zote mbili. Kwa mfano binti wa Kipsigis kuolewa na mwanamume wa Abagusii na au binti wa Abagusii kuolewa na mwanamume wa Kipsigis. Kando na ndoa, biashara, urafiki, shughuli za kijamii kama vile matanga na maeneo ya burudani kama vile mikahawa ni baadhi ya nyenzo zinazotumiwa na wanajamii hawa kuimarisha uhusiano wao na kuendeleza amani na utulivu.

**Mfano 30:**

***Mtf:*** *okay kitu ambayo imekuwa ikisababisha muelewane na hawa ni nini?*

***Daniel Kimosop:*** *kuelewana hapa ilianza kwa kuoana.*

Ndoa kati ya jamii mbili au zaidi ambazo kwa kawaida huwa na mitafaruku huwa kama suluhisho na chanzo cha mlahaka mwema kati ya jamii hizo (Kioko & Bollig, 2015). Waligundua hayawalipotafiti ndoa na ubadilishanaji ardhi kama vigezo vya kuimarisha mahusiano kati ya jamii ya Maasai na Kikuyu katika jimbo ndogo la Naivasha, eneo la Maiela na Enoosupukia, mpaka wa jimbo la Nakuru na Narok. Ndoa kati ya jamii ya Maasai na Kikuyu katika maeneo haya iliimarisha mahusiano kati ya jamii hizi mbili na kupunguza mitafaruku iliyokumba jamii hizi. Hata hivyo ni wasichana wengi wa jamii ya Kikuyu ndio waliolewa na wanaume wa Kimaasai ikilinganishwa na idadi ya wanaume wa Kikuyu waliooa mabinti wa Kimaasai. Matokeo haya yanafanana na matokeo ya utafiti huu. Ithibati ikiwa katika mfano 30, ambapo mzee kutoka jamii ya Kipsigis alieleza kuwa chanzo cha amani kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis ni ndoa. Ndoa ni muhimu miongoni mwa jamii hizi kwani hali hii hukuza uhusiano mwema na hivyo basi kuleta suluhu kati yao. Matumizi ya majina ya urejelezi kama vile *Korera*, *Omwabo Omosani* miongoni mwa jamii ya Abagusii, na *Batieb* na *Bomori Ahure* miongoni mwa Kipsigis hupunguza uwezekano wa vita kutokea kwa sababu kunapokuwa na vita, hata jamaa zao waliolewa upande ule mwingine wataumizwa na huenda hata kukawa na vifo.

**Mfano 29:**

***Mtf:*** *Na wazee wakiwa marafiki?*

***1.Mzee Meto Arap Koech:*** *hiyo you know when this word applies, ya marriage, mtu wa heshima bomori hata kama watoto hawajaoana*

***Mtf:*** *Sasa wakati mwingine kwa mfano ule wa matanga, na kunaurafiki?*

***2. Mzee Meto Arap Koech:*** *Enyewe when there’s a burial wanaattend siku hizi hata iwe ndani ya maeneo yao.*

***Mft:*** *How do you refer to them?*

***3.Mzee Meto Arap Koech:si abasani, marafiki***

***Mft:*** *marafiki ni Kiswahili*

***4.Mzee Meto Arap Koech:*** *Ama Ahule, Kamama. Hawa ni watu wamoja so wanaamsha wote waongee.*

***5.Moses Arap Rotich:*** *Kamama usually covers a wide range*

***(Kiambatisho Y:24/3/2022)***

Tabia za kiurafiki kwa watu wengine inaweza kuimarisha baadhi ya mambo katika utangamano na watu mojawapo ikiwa usuluhishaji wa vurugu na mitafaruku kati ya watu (De Wied na wenzake, 2007). Wanaongezea kuwa, urafiki huimarisha maelewano kati ya watu na hivyo kuzuia tabia hasi zinazoweza kusababisha huharibifu na kuimarisha tabia chanya zinazoweza kuimarisha hali ya amani na utulivu. Maelezo haya yanaingiliana na matokeo ya utafiti huu. Katika mfano 31, mzee kutoka jamii ya Kipsigis anaeleza kuwa huwa kuna urafiki kati ya wazee kutoka upande wa Kipsigis na Abagusii. Urafiki huu huimarishwa kupitia matumizi ya istilahi za urejelezo kama vile *bomori*. Hii ni kwa sababu jina hili ni jina la kiheshima ambalo hutumiwa tu na watu ambao watoto wao wameoana. Mzee wa jamii ya Kipsigis, anaeleza kuwa ingawa huwa watoto wao hawajaona lakini wanatumia istilahi hii kurejeleana kama ishara ya urafiki na heshima. Urafiki huu unaweka msingi wa kusuluhisha aina yoyote ya matatizo kati yao. Pia urafiki huu hivyo unajenga utangamano bora, wenye utulivu na amani.

Urafiki anaozungumzia Mzee huyu pia unatuonyesha matokeo yake. Kwamba kwa kuwa kuna urafiki kati ya wanajamii wa Kipsigis na Abagusii, iwapo kuna shughuli kama vile matanga, wanajamii wote watahudhuria. Anasema kwamba siku hizi hata matanga iwe ndani kiasi gani, wanajamii wa Kipsigis wanahudhuria. Kwenda 'ndani hata iwe kiasi gani' ni ishara kuwa kuna uaminifu wa usalama. Kwa kuwa wanahakikisho la usalama, siku hizi hawana woga wa kwenda kujumuika na watu wa jamii ya Abagusii katika shughuli hizi. Kwamba wanajamii hawa wanaweza kuhudhuria hafla kwa pamoja ni ishara ya suluhisho ya vurugu kati yao. Ni ishara kuwa hata iwapo patakuwepo na ghasia kwa kiasi fulani, bado sherehe na shughuli za kijamii zitawaleta pamoja hivyo kuwaunganisha na kuwasaidia kusuluhisha tofauti zao.

**Mfano 30:**

***Mft:*** *nyinyi mnaingia kwao?*

***1.Moses Gichana:*** *wanajitenga*

***2.Antony Kibagendi:*** *lakini wewe huoni pale kwenye tunakunywa chai*

***3.Moses Gichana:*** *wanajitenga*

***4.Antony Kibagendi:*** *hawa wanakuja wanakaa kwa hii meza na wale kwa ile lakini wanapiga stori*

***(Kiambatisho Z (1):25/3/2022)***

Katika mfano 30 hapa juu, vijana wa jamii ya Abagusii wanalalamika kuwa wenzao kutoka jamii ya Kipsigis hujitenga hata katika mikahawa. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa ingawa wanajitenga, angalau huwa wanakua pamoja, katika mkahawa moja. Kinachowatenganisha huwa tu mtindo wa kuketi. Kwambla wanajamii wa Abagusii hukaa katika upande mmoja wa mkahawa ilhali wanajamii wa Kipsigis huwa wamekaa katika upande mwingine wa mkahawa. Hali hii mtafiti pia alishuhudiakatika kipindi alichokaa nyanjani. Huenda hii ni tabia hasi inayoleta mgawanyiko kati ya jamii hizi mbili, kwani wote wamekwisha kubali na kuridhia hali hii. Kwa hivyo tabia haichukuliwi tena kuwa hasi, bali ni mtindo wao wa utangamano (Kimetto, 2022). Ingawa wanajamii hawa hawakai pamoja, wakati huo wa kula huwa wanazungumza Kiswahili na kupiga gumzo kama watu wanaojuana. Hii ni ithibati kuwa kule kukutana kwenye mkahawa ni tukio la utangamano ambalo huchangia katika kupoesha hali yoyote ya mitafaruku kati ya wanajamii hawa. Pia ni tukio linaloonyesha kuwa ni njia moja inayochangia katika amani na utulivu uliopo katika jamii hizi mbili.

**Mfano 31:**

***1.Antony Kibagendi:*** *ni kama hawapendi kutangamana*

***2.Moses Gichana:*** *jambo lingine katika soko zetu ukweli kuanzia 2007 kwa ile clashes hapo kuelekea nyuma miaka ile ya nyuma hakukuwa na wakale ambao walikuwa wakifanya biashara upande wa Kisii. Lakini nowadays tangu 2007 mpaka sasa sijui kitu gani wameona. Enyewe ukienda kwa masoko zetu unawapata wanauza maziwa. Zamani tulikuwa tunabeba tunapeleka sisi wenyewe lakini*

*wao hawakuwa wanaenda lakini siku hizi wanaenda, uende sehemu za Sotik. Kapkatet, Tanai. Siku hizi wanatoa vitu Kisii. Hii enyewe tumewawekea tick.*

***(Kiambatisho Z (2):25/3/2022)***

Mojawapo ya rasilimali inayotumiwa kwa pamoja na jamii ya Abagusii na Kipsigis ni soko. Soko hii ipo katika pande zote za barabara katika mpaka wa Chebilat. Kulingana na maelezo ya mshiriki kutoka jamii ya Abagusiikatika mfano 33 hapo awali, kabla ya mwaka wa 2007, wanajamii wa Kipsigis hawakufanya aina yoyote ya biashara kwa upande wa Abagusii. Ikumbukwe kuwa hapo mpakani Chabilat upande wa juu ni Kipsigis yaani Kaunti ya Bomet ilhali upande wa chini ni kwa Abagusii, Kaunti ya Nyamira. Hii ni kumaanisha kuwa kabla ya mwaka wa 2007 wanajamii wa Kipsigis walifanya biashara kwa upande wao pekee. Hawakuvuka barabara kuelekea upande wa Abagusii. Hata hivyo wakati huo na hata sasa, wanajamii wa Kipsigis wanaingia na kufanya biashara upande wa Abagusii. Wanajamii wengine wa Abagusii hata wananunua mashamba upande wa Kipsigis na kujenga boma zaohuko. Hali hii si sawa na jamii ya Kipsigis. Ilikuwa ni vigumu kupata mwanajamii wa Kipsigis akivuka upande wa Abagusii kufanya biashara au hata kuishi upande ahuo. Hii ni ithibati kwamba kuna dhana ya amani na utangamano kati ya jamii hizi kwani kuna matumizi ya urejelezi kama vile *Omosani, Oyonka, Batieb, Bomori* na *Kamama* kutoka jamii zote wanaposhiriki biashara.

Baada ya ghasia za kisiasa za mwaka wa 2007 ni kana kwamba, wanajamii hawa waligundua umuhimu wa ushirikiano, amani na mlahaka mwema. Hii ndio njia pekee ya kuelezea mabadiliko ambayo yalitokea miongoni mwa wanajamii kujihusisha katika biashara upande ambao unachukuliwa kuwa wa Abagusii. Mtafiti alipokuwa nyanjani, aliweza kuonyeshwa baadhi ya majengo ambayo yamechipuka hivi majuzi na ni wazi kuwa wanajamii wa Kipsigis wamefungua biashara upande wa Abagusii. Hii inaonyesha wazi kuwa kuna amani na utangamano kati ya jamii hizi mbili ambazo zimekuwa na uhasama miongoni mwao kwa kipindi kirefu kutokana na matumizi ya lugha ya urejelezi kati yao. Wanajamii wa Abagusii pia wamefanya vivyo hivyo upande ule mwingine ambao unachukuliwa kuwa wa Kipsigis.

Inasemekana kuwa wanajamii wa Kipsigis siku hizi wanavuka na kuuza maziwa, mifugo na bidhaa nyinginezo katika upande wa kaunti ya Nyamira. Kutumia soko hili kwa pamoja ni

ishara ya uhusiano mwema. Ni ishara ya kuwa wanajamii hawa wangependa kuishi pamoja ingawa wanatofautiana kikabila. Hali hii ni ithibati kuwa licha ya mitafaruku kati ya jamii hizi kunambinu za suluhisho zinazotumiwa na Abagusii na Kipsigis kuunda uhusiano bora kati yao (Mwanzi, 1977). Matumizi ya soko kwa pamoja na watu wote kutoka jamii zote mbili kufanya biashara kwa pamoja imetumiwa kama mbinu ya kukabiliana na uhasama miongoni mwa jamii hizi mbili. Ni mbinu ya kusuluhisha tofauti zao kwa sababu wanatumia wateja kwa pamoja. Pia kila mmoja amewekeza katika eneo hili na hivyo iwapo kutatokea vurugu kila mtu atapata hasara kiuchumi. Kwa misingi hii, uwekezaji na ufanyaji biashara kwa pamoja inawapa utulivu wa kiasi fulani, ikiambatanishwa na heshima, mlahaka mwema na amani. Ni wakati huu wa kufanya biashara kwa pamoja urejelezi wa majina kama vile *Omosani, omonyamato, oyonka, Omoibori miongoni* mwa jamii ya Abagusii na *Kamama, Nyamutio, Bomori, Batieb, Gosebine* miongoni mwa Kipsigis utumiwa.

**4.5 Hitimisho**

Jamii za Abagusii na Kipsigis wana matumizi ya urejeaji na mahusiano kati yao. Matumizi ya urejelezi huu husababisha rabsha na hata vita. Katika matumizi haya ya urejelezi kati ya jamii hizi kunamalengo ambayo wanakusudia kuafiki kama jamii. Katika kurejeleana kuna dhana hasi na chanya. Wana majina na istilahi za kurejeleana katika misimu yote ile; msimu wa furaha ambapo wao hukusanyika pamoja na sherehe kusheni, ambapo urejelezi huwa ni kama *Batieb, Bomori*, *Kamama*, *Omosani*, *Korera*, *Omoibori*, msimu wahuzuni, ghasia ambapo urejelezi huwa ni kama vile *Nyamutio*, *Bunyo*, *Gosebinde* na kadhalika na wakati wa utulivu. Matumizi haya ya lugha rejelezi yana athari hasi na chanya katika mahusiano yao. Lugha rejelezi hudumisha amani kwa kujua au kutojua na wakati huo huo pia huzua hasira na hata vita kwa kuwa moja jamii huhisi kuwa jamii nyingine inatumia urejelezi huu kwa nia ya kuwadunisha. Kadri muda ulivyokwenda, wanajamii hawa wamejifunza kuishi katika eneo hili kwa amani na utulivu kupitia ndoa, biashara na matumizi ya rasilimali walizonazo kwa pamoja. Hali hii huleta suluhu na amani kati ya jamii hizi za Abagusii na Kipsigis.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ndiyo tamati ya kazi hii inayoshughulikiautafiti huu pasi na kusahau deta ilivyokusanywa na matokeo ya utafiti. Sehemu ya hitimisho imefafanua matokeo ya utafiti kwa ujumla na hatimaye mafanikio na mapendekezo yanayotokana na kazi.

## 5.2 Muhtasari

Tasnifu hii ina jumla ya sura tanoambazo ni hitimisho, lugha ya urejelezi miongoni mwa Abagusii na Kipsigis, athari za lugha ya urejelezi katika mahusiano ya jamii ya Abagusii na Kipsigis, mbinu za suluhisho zinazotumiwa na Abagusii na Kipsigis kuimarisha uhusiano, mafanikio ya utafiti, matatizo ya utafiti namapendekezo kuhusu mizozo kati ya jamii hizi mbili.

## 5.3Hitimisho

Baada ya utafiti, mambo mbalimbali yaligunduliwa kuhusu uhusiano wa jamii ya Abagusii na Kipsigis kwa misingi ya lugha wanayotumia kurejeleana. Matokeao haya yametokana na maelezo ya washiriki walioshirikishwa kwenye utafiti.

### 5.3.1Lugha ya Urejelezi miongoni mwa Abagusii na Kipsigis

Utafiti huu ulichunguza lugha ya urejelezi inayotumiwa na Abagusii kuwarejelea Kipsigis na ile inayotumiwa na jamii ya Kipsigis kuwarejelea Abagusii. Mfano wa isitilahi za urejelezi za kijumla ni kama vile *Ongora*, *Bwongobwongo*, *Omworo*ni istilahi inayotumiwa na Abagusii kurejelea binti wa Kipsigis.*Omworo* hurejelea mwanamke ambaye hufanya kazi yake polepole sana. Vijana wa Abagusii wanafananisha na mvivu hivi lakini ni mwanamke anayefanya kazi bila haraka yoyote. Kulingana na washiriki haiwezekani kupata*omworo*katika jamii ya Abagusii.

*Omworo* ambao wakati mwingine huitwa *chorire* pia ina maana ya mwanamke mpole asiye na mambo mengi kama vile kelele hivi na ugomvi. Wanawake wa Kipsigis wanajulikana kwa jina hili kwani wao huwa wapole, hukwepa ugomvi hata na waume wao na huwa wakarimu.

Kwa upande mwingine mwanamke wa jamii ya Abagusii akiolewa katika jamii ya Kipsigis hurejelewa kama *teinge* yaani tingatinga kwa sababu wao hufanya kazi kwa nguvu na bidii. Pia anaweza kurejelewa kama *bwangobwango* yaani mtu anayefanya kazi yake kwa haraka.
Lugha ya urejelezi katika jamii ya Kipsigis na Abagusii hutumika kwa kutegemea misimu mbalimbali kama vile misimu ya ndoa, furaha na urafiki.

Uhasama miongoni mwa jamii ya Abagusii na Kipsigis hutokea kwa sababu ya wizi wa mifugo na wakati wa siasa. Vijana wanaokwenda kuiba mifugo hutumia neno mahususi ili kutenga aliye mmoja wao na asiye mmoja wao. Istilahi ya urejelezi iliyojitokeza kwa wingi wakati wa uhasama ni *bunyo*. Ni neno lenye asili ya Kipsigis. Hutumiwa na Kipsigis kurejelea jamii ya Abagusii. Pia hutumiwa kuwarejelea Abagusii kama neno la kijumla linalomaanisha adui. Wakati *bunyot* ni istilahi ya urejelezi inayotumiwa na Kipsigis kurejelea Abagusii wakati wa uhasama, kwa upande wa Abagusii wanawarejelea Kipsigis kama *omobisa* wakati wa uhasama.Katika jamii ya Abagusii, neno lingine linalotumiwa kuwarejelea Kipsigis wakati wa uhasama au wakati wa usiri katika mazungumzo ni *omonyamato* kumaanisha mtu aliyetolewa masikio. Jamii ya Kipisigis wana ufahamu kuwa Abagusii huwaita huwarejelea hivi na kila wanaposikia jina hilo wao hukasirika.

Jina *omurumbwa* pia hutumiwa na Abagusii kuwarejelea Kipsigis. Hata hivyo, jamii ya Kipsigis hawapendi jina hili na kuchukulia kuwa ni linamaanisha mbwa. Hata hivyo maelezo ya wazee walioshiriki utafiti huu yalionyesha chanzo cha jina hili *omurumbwa*. Ni jina lilitokana na kiapo kati ya jamii ya Kipsigis na wazungu ili kuafikia kikomo cha vita kati ya wazungu na jamii ya Kipsigis.

Kuna baadhi ya urjeleziambao ukitumiwa huwa kama uchokozi na hivyo wanajamii wa Kipsigis na Abagusii wanaporejeleana kwa kutumia urejelezi huo hupandwa na hasira. Urejelezi huu una msingi wake katika utamaduni wa kutahiri. Jamii ya Kipsigis na Abagusii wote hutahiri vijana wao wa kiume wanapofika umri wa uzulufu. Istilahi za urejelezi kama vile *ngetai, ngete, omoisia* zinapotumiwa miongoni mwa vijana wa kiume huzua rabsha na huwa ishara ya uchokozi. Anayerejelewa kwa kutumia istilahi hizi hukasirika. Miongoni mwa wanawake istilahi ya urejelezi zinazozua hasira ni *egesegene* upande wa Abagusii na *chepto* upande wa Kipsigis. Hata hivyo istilahi hizi za wanawake zinaacha kutumika kutokana na

marufuku ya kuwatahiri wanawake. *Ngetai, ngete* na *Omoisia* ni isitilahi za Kipsigis na Abagusii mtawalia zinatumiwa na jamii hizi kurejeleana kwa hali ya uchokozi au uhasama. Istilahi hizi zinamaanisha mtu ambaye hajatahiri. Kutahiri ni mojawapo ya njia ya utambulisho katika jamii hizi mbili kama inavyoelezea nadharia utambulisho wa kabila.

Katika msimu wa utulivu ambao ndio muda mrefu ikilinganishwa na msimu wa uhasama istilahi maarufu ya urejelezi katika jamii zote mbili ni *kamama*. Ingawa istilahi hii ya urejelezi inatumiwa kurejeleana katika pande zote, asili yake inajikita sana katika jamii ya Kipsigis. *Kamama* kulingana na jamii ya Kipsigis wanachukulia jamii ya Abagusii kama mama yao. *Kamama* ni istilahi yenye uzito, kwani hutumiwa kama chombo cha kuleta amani. Wakati wa uhasama au vita katika jamii hizi mbili, *kamama* hutumiwa kama istilahi shawishi ili kutuliza hali na kupunguza joto ya uhasama.

Matumizi ya istilahi rejelezi *Kamama* iliunda msingi wa uhusiano mwema kati ya jamii ya Kipsigis na Abagusii. Uhusiano huu umeendelea mpaka sasa hivi kwamba hata kizazi cha sasa kinajua matumizi yake na wanaelewa matumizi na chanzo chake. Istilahi rejelezi yenye urafiki ni *gosobe/gosobinde*. *Gosobe/bosobe*inasemekana ni ufupisho wa *bosobinde* au *gosobinde*. Isitilahi hizi hutumiwa na jamii ya Kipsigis kurejelea jamii ya Abagusii. Vijana wa Abagusii huchukulia kuwa istilahi hizi zinamaanisha *Mkisii* yaani anayezungumza lugha ya Ekegusii. Isitilahi miongoni mwa jamii hizi mbili ni jambo la kawaida, inayotumiwa wakati wowote bila kuzua rabsha, vurugu au vita. Jamii ya Abagusii wanarejelewa kwa istilahi hizi na hawana tatizo na wameizoea.

Ingawa *gosobe/bosobe* na *gosobinde/bosobinde* inachukuliwa na vijana kumaanisha *Mkisii*, kuna maana nyingine ambayo inajificha katika historia. Ni maana ambayo wazee tu wanaijua ama kuielewa. Istilahi hizi zimekubalika miongoni mwa vijana na wazee ila ni wazee wanaoelewa maana kamili ya istilahi hizi. Wazee wanaeleza kuwa Istilahi *gosobinde* inamaanisha mponyaji, yaani mtu wa jamii ya Abagusii walioponya jamii ya Kipsigis walipokuwa wanakufa kutokana na magonjwa. Ujio wa *gosobinde* vilevile kama *kamama* ikajenga msingi wa uhusiano mwema kati ya jamii ya Kipsigis na Abagusii.

*Omoyega* ni istilahi inayomaanisha furaha na hutumiwa katika kipindi chochote kile cha msimu wa furaha na misimu ya sherehe mbalimbali kama vile harusi, kutoa vijana jandoni na sherehe zozote zile za furaha. Ni istilahi rejelezi inayotumiwa na jamii zote mbili.
Kumekuwepo na utangamano kati ya jamii hizi mbili katika kiwango cha ndoa. Istilahi za urejelezi wakati huu ni kama vile *Batiem*na *Bomori*ambazo hutumiwa na jamii ya Kipsigis kuwarejelea Abagusii ilhali *Korera* na *Abule*hutumiwa na jamii ya Abagusii na Kipsigis mtawalia kurejelea jamii ya Abagusii na Kipsigis. Hizi ni istilahi zinazotumiwa na wazee ambao watoto wao wameoana.

Iwapo mwanaume/mvulana wa Abagusii anaoa msichana kutoka jamii ya Kipsigis, wazazi kutoka jamii ya Abagusii urejelea *korera*, istilahi ambayo hutumuwa kurejelea wazazi wa mamake binti aliyeolewa. Kwa upande wa Kipsigis ataitwa *Batiem ama Abule*. Istilahi ya mwanamke/msichana wa jamii ya Kipisigis, babake huyo msichana atarejelewa kama *Bomori*na mama *Batieb*. Matumizi haya hutumiwa na jamii hizi mbili kurejeleana hadi imekuwa mazoea hivi kwamba ni vigumu kujua iwapo asili ya istilahi hizi ni lugha ya Abagusii au Kipsigis. Jamii ya Kipsigis wanamwita mama wa binti ya Abagusii aliyeolewa miongoni mwa Kipsigis *Batieb* ama *Korera*.

Urafiki miongoni mwa jamii ya Abagusii na Kipsigis ina misingi yake katika maelezo ya visasili. Hivyo wamekuwa na mahusiano ya urafiki kwa muda mrefu. Istilahi kama vile *Bomori na korera*hutumiwa miongoni mwa wazee. *Bomori*na *Korera*hutumiwa miongoni mwa wazee ambao watoto wao wameoana. Hata hivyo yanatumiwa vilevile miongoni mwa wazee wa jamii ya Kipsigis na Abagusii ambao ni marafiki kurejeleana. Majina mengine ya urafiki hasa miongoni mwa vijana ni *omosani* ama *Minto*.*Minto* ni istilahi rejelezi yenye maana ya “mtu wetu” miongoni mwa jamii ya Abagusii.

### 5.3.2 Athari za Lugha ya Urejelezi katika Mahusiano ya Jamii ya Abagusii na Kipsigis

Athari hasi katika muktadha wa utafiti huu ni vita. Vita na mitafaruku kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis huwa haisababishwi na mambo makubwamakubwa bali ni mambo madogo kama isitilahi rejelezi ambazo zitachukuliwa kuwa ni matusi na wazungumzaji. Katika hali hii, istilahi iliyotolewa na mtu mmoja inaweza kuzua vita kati ya watu wa jamii tofauti. Vita hivi vinakuwa kwa misingi ya ‘mwenzetu’ ama ‘mtu wetu’ ametukanwa. Bali ni kwa misingi kuwa

‘mkisii mwenzako’. Yaani ‘sisi’ ambao hapa ni Abagusii tumechokozwa na ‘wao’ ambao hapa ni Kipsigis. Ugomvi unaacha kuwa kati ya mtu na mwingine na kuwa kati ya jamii moja dhidi ya jamii nyingine.

Vijana wa jamii ya Abagusii wanaainisha majina ya urejelezi ambayo wanajua jamii ya Abagusii hutumia kurejelea jamii ya Kipsigis. Majina haya wakati mwingi huzua vita mingoni mwa vijana hasa wanapogundua matumizi ya urejelezi huo una maana hasi.

Hata hivyo, kuna uhusiano na mlahaka mwema kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis. Jamii zote mbili hazionyeshi dalili za uhasama wa aina yoyote. Mtafiti aligundua kuwa katika maeneo ya burudani kama baa na maakuli kama hoteli jamii hizi mbili zilitangamana japo kwa uangalifu. Wateja wa kutoka jamii Abagusii walikaa upande mmoja ilhali wale wa kutoka jamii ya Kipsigis pia walikaa upande mwingine. Kule kujitenga kunaonyesha kuna tofauti za kindani mno ambazo huenda zisizungumziwe waziwazi, lakini yanaongoza mahusiano na utangamano wa jamii hizi mbili.

Kulikuwa na madai kuwa wanajamii wa Kipsigis wanafunzwa utambulisho wao kikabila wakiwa bado watoto. Hivyo wanapokuwa watu wazima wanajua tofauti yao na jamii ya Abagusii na wanajua tofauti kati yao kama jamii moja na jamii ya *gosobe*. Kijana wa jamii ya Abagusii anaeleza kuwa utambulisho huu unatambuliwa hata na watoto wadogo. Jamii ya Abagusii na Kipsigis wana utamaduni wa kutahiri watoto wao wanapobaleghe, hasa watoto wa kiume. Mwanaumeambaye hajatahiri huchukuliwa kuwa na kasoro. Urejelezi wa mtu ambaye hajatahiri unapotumiwa kurejelea mwanamume wa Abagusii na Kipsigis ambaye ametahiri huzua mizozo. Kwa mfano, kama inavyoelezewa na washiriki, iwapo wanajamii wa Abagusii watarejelea mwanaume wa Kipsigis kwa kumuita urejelezi *ngetai* au *ngeta* basi hiyo itakuwa chanzo cha vita. Wanajamii wa Kipsigis pia wanapomrejelea mwanaume wa Abagusii kwa kumuita *Omoisia,* ni uchokozi. Hii huzua mizozo na kuwakasirisha sana watu wa Abagusii. Wanajamii hawa wote wanajua mathara ya istilahi hizi kwni matumizi yazo yana mipaka.

Hali hii pia ni sawa miongoni mwa wanawake. Wakati ule ambao utamaduni wa kutahiri wanawake ulipokuwa, kumuita mwanamke wa Kipsigis *chepto* inaweza kuzua vita miongoni mwa wanawake wa Kipsigis. Hali hiyo ni sawa na wanajamii wa Abagusii. Kurejelea

mwanamke wa Abagusii *egesagane* itazua mizozo. Kwa sababu neno hili linamaanisha mwanamke ambaye hajatahiriwa.

Jina *omonyamato* miongoni mwa Kipsigis inamaanisha mtu ambaye ametobolewa masikio. Hapo zamani mojawapo ya tamaduni ya Kipsigis ilikuwa kutobolewa masikio. Kwa sasa ni utamaduni ambao ulizikwa katika kaburi la sahau. Leo hii iwapo wanajamii wa Abagusii watatumia istilahi hii kuwarejelea wanajamii wa Kipsigis, basi huzua vita na migogoro.

Matumizi ya lugha rejelezi ina athari hasi katika jamii hizi mbili zinazopakana na wakati huo huo ni majirani wanaotumia rasilimali kadhaa kwa pamoja. Ni muhimu kutaja kuwa, washiriki kutoka upande wa Abagusii walikuwa na mengi ya kusemi ili kuonyesha athari hizi. Hata hivyo, vijana wa jamii ya Kipsigis hawakuwa na chochote cha kusema. Hili huenda lilichangiwa na ukweli kuwa mtafiti vilevile ni wa jamii ya Abagusii. Kwa sababu mtafiti alikuwa wa jamii ya Abagusii, huenda washiriki kutoka jamii ya Kipsigis walihisi kuwa mtafiti alikuwa si wa kwao na hivyo hawakuona haja ya kutoa habari muhimu alizohitaji mtafiti.

Lugha ya urejelezi inaweza kuwa na athari hasi. Kando na kusababisha mizozo inaweza kuwafanya wazungumzaji na warejelewa kuingia katika vita vikali. Hata hivyo si wakati wote ambapo lugha ya urejelezi husababisha mambo mabaya. Lugha ya urejelezi inaweza kuwa na athari chanya, inaweza kuzua mambo mazuri miongoni mwa wanaotumia lugha hiyo. Lugha ya urejelezi unaweza kuimarisha uhusiano wa wanajamii kwa njia nzuri na hivyo kutumiwa kujenga uhusiano miongoni mwa wanajamii.

Wanajamii wa Kipsigis na Abagusii huitana *kamama*. Ni jina ambalo limetumiwa kwa muda mrefu sana na wanajamii hawa. Ili kukabiliana na njaa, wanajamii wa Kipsigis waliomba chakula kutoka kwa Abagusii. Nao baadhi ya watoto wa kike wa Kipsigis wakapeanwa kwa Abagusii. Ikawa ni hali ya kubadilishana watoto kwa chakula. Kwa sababu hii, kulingana na washiriki kuna jamii ya Kipsigis wengi Nyamira, miongoni mwa Abagusii. Panapotokea vurugu kati ya Kipsigis na Abagusii, mara nyingi vita hivyo hukomeshwa kwa kukumbushana historia na matumizi ya istilahi *kamama*. Matumizi haya huwa ni istilahi inayojaribu kudokeza kuwa wao ni jamaa na hivyo hakuna haja ya kupigana.

Watoto wa kisasa wa Abagusii na Kipsigis hawajui maana ya *gosobinde.* Hata hivyo *gosobinde* ni neno ambalo lina historia ndefu na yenye kuonyesha asili ya uhusiano mwema kati ya Kipsigis na Abagusii. Wazee hawa wanasema kuwa jina hili lilitokana na hali ya Abagusii kuwasaidia kwa kuwatibu walipokuwa wanakumbwa na magonjwa. Abagusii walikuwa waganga waponyaji ambao walitoa huduma za uponyaji wa Abagusii na Kipsigis. Wanajamii wa Kipsigis walipouwawa katika vita na jamii zingine, Abagusii wangeenda kuchukua miili yao na kuwasaidia wale ambao walikuwa wameumizwa vibaya. Kuanzia wakati huo, kumekuwa na uhusiano mwema, kwa sababu Abagusii ni waponyaji wao.

### 5.3.3Mbinu za Suluhisho Zinazotumiwa na Abagusii na Kipsigis Kuimarisha Uhusiano

Utafiti huu uliangazia lugha iliyotumiwa na washiriki hivyo mbinu za suluhisho ziliainishwa kutoka kwa mazungumzo ya washiriki. Kutokana na mazungumzo kati ya mtafiti na washiriki, ilibainika kuwa migogoro kati ya Abagusii na Kipsigis ilikomeshwa na uwepo wa ndoa kati ya wanajamii kutoka jamii zote mbili.

Ndoa kati ya jamii mbili au zaidi ambazo kwa kawaida huwa na mitafaruku huwa kama suluhisho na chanzo cha mlahaka mwema kati ya jamii hizo (Kioko & Bollig, 2015). Chanzo cha amani kati ya jamii ya Abagusii na Kipsigis ni ndoa. Ndoa inapotokea kati ya jamii hizi mbili hupunguza uwezekano wa vita kutokea kwa sababu kunapokuwa na vita, hata jamaa zao waliolewa upande ule mwingine wataumizwa na huenda hata kukawa na vifo.

Urafiki kati ya wana jamii wa Kipsigis na Abagusii hasa wazee huimarishwa kupitia matumizi ya istilahi za urejelezi kama vile *bomori na korera*. Hii ni kwa sababu majina hayani majina ya kiheshima ambayo hutumiwa tu na watu ambao watoto wao wameoana. Urafiki huu unaweka msingi wa kusuluhisha aina yoyote ya matatizo kati yao. Pia urafiki huu unajenga utangamano bora.

Kwa kuwa kuna urafiki kati ya wanajamii wa Kipsigis na Abagusii, iwapo kuna shughuli kama vile matanga, wanajamii wote huhudhuria kwa sababu kuna hakikisho la usalama. Wanajamii hawa kuweza kuhudhuria hafla kwa pamoja ni ishara ya suluhisho ya vurugu kati yao. Ni ishara kuwa hata iwapo patakuwepo na ghasia kwa kiasi fulani, bado sherehe na shughuli za kijamii zitawaleta pamoja na hivyo kuwaunganisha na kuwasaidia kusuluhisha tofauti zao.

Vijana mara nyingi huwa wanakula pamoja, katika mkahawa moja. Kinachowatenganisha huwa tu mtindo wa kuketi. Wanajamii wa Abagusii hukaa katika upande mmoja wa mkahawa ilhali wanajamii wa Kipsigis huwa wamekaa katika upande mwingine wa mkahawa. Bila kuchunguza kwa undani, inaonekana kuwa tabia hasi inayoleta mgawanyo kati ya jamii hizi mbili, lakini ni wazi kuwa katika utangamano wa muda, wote wamekwisha kubali na kuridhia hali hii. Kwa hivyo tabia haichukuliwi tena kuwa hasi, bali ni mtindo wao wa utangamano.

Soko la Chebilatlinatumiwa kwa pamoja na jamii ya Abagusii na Kipsigis. Kabla ya mwaka wa 2007, wanajamii wa Kipsigis hawakufanya aina yoyote ya biashara kwa upande wa Abagusii. Hii ni kumaanisha kuwa kabla ya mwaka wa 2007 wanajamii wa Kipsigis walifaya biashara kwa upande wao pekee. Hawakuvuka barabara kuja upande wa Abagusii. Baada ya ghasia za kisiasa za mwaka wa 2007 ni kana kwamba, wanajamii hawa waligundua umuhimu wa ushirikiano, amani na mlahaka mwema. Inasemekana kuwa wanajamii wa Kipsigis siku hizi wanavuka na kuuza maziwa, mifugo na bidhaa nyinginezo katika upande wa kaunti ya Nyamira. Kutumia soko hili kwa pamoja ni ishara kuwa wanajamii hawa wangependa kuishi pamoja ingawa wanatofautiana kikabila na kiutamaduni.

### 5.3.4 Mafanikio ya utafiti

Utafiti huu umefaulu kuonyesha kuwa matumizi ya lugha ya urejelezi ni jambo la kawaida katika jamii jirani. Utafiti huu ulifanikiwa kuonyesha lugha ya urejelezi miongoni mwa Abagusii na Kipsigis. Istilahi hizi za urejelezi zinatumika katika misimu mbalimbali. Kuna zile zinazotumiwa misimu ya furaha, urafiki na sherehe. Zingine zinatumika wakati wa uhasama na migogoro.

Utafiti huu pia umefanikiwa kueleza athari za lugha ya urejelezi inayotumiwa na Abagusii na Kipsigis kurejeleana. Lugha ya urejelezi inaweza kuwa uchokozi, hivyo kuishia kuzua hasira na mzozo kati ya wanajamii hawa. Lugha ya urejelezi pia inatumiwa kudumisha amani na kuimarisha uhusiano wa jamii hizi mbili.

Utafiti umefaulu kuonyesha kuwa jamii zenye mizozo zinapotumia rasilimali kwa pamoja na kufanya biashara pamoja, huwa wanapata kusuluhisha tofauti zao na kudumisha amani. Utafiti pia umeweza kuthibitisha kuwa chanzo kikuu cha kupatikana na kudumishwa kwa amani kati ya jamii zinazohitilafiana ni ndoa.

### 5.3.5 Matatizo ya utafiti

Utafiti huu ulikumbwa na matatizo mbalimbali:

Kuaga kwa wasailiwa: Baadhi ya wasailiwa hasa wale ambao ni wazee wenye umri mkubwa, ambao walikuwa na historia muhimu waliaga dunia kati ya kipindi cha utafiti wa awali na utafiti wenyewe. Kwa mfano mzee wa jamii ya Kipsigis, mwenye umri wa miaka 98, aliyeaminika kuwa na historia na deta bora aliaga dunia siku ambayo mtafiti alifika nyanjani. Pia, mtafiti aliarifiwa kuwa mzee wa Abagusii aliaga dunia juma iliyotangulia kabla ya mtafiti kufika nyanjani. Hili lilikuwa changamoto ambayo mtafiti hakuwa na udhibiti wowote au njia yoyote ya kuisuluhisha. Mtafiti alitatua suala hili kupitia msaada wa chifukutoka sehemu hizi ambao walipendekeza wazee wengine ambao walifanikisha ukusanyaji wa deta aliyohitaji mtafiti.

Tatizo lingine lilikuwa lugha, hasa upande wa jamii ya Kipsigis. Kwa sababu mtafiti hakuwa na umilisi wa lugha ya Kipsigis, ilikuwa vigumu kufanya mahojiano kikamilifu na yenye kuzua deta bora. Kukabiliana na hili, mtafiti, kupitia chifu, alipata kijana wa Kipsigis, aliyemsaidia kuzungumza na wanajamii wa Kipsigis wakati wa mahojiano katika vikundi viini. Hata hivyo, kijana wa Kipsigis aliyetumika kuzugumza lugha hiyo kwa niaba ya mtafiti mara nyingi alikosa kuelewa maswali ya mahojiano. Aliishia kuuliza wasailiwa maswali visivyo, hivyo kuzuia upatikanaji wa deta. Mtafiti alijaribu kuzungumza na wasailiwa kwa lugha ya Kiswahili huku maswali na majibu yakifanyiwa tafsiri. Vijana na hasa kutoka jamii ya Kipsigs hawakushiri utafiti kwani ni wachache tu ambao walishiriki kwa jumla wazee 80%kina mama 70% walioshirik na vijana 40%.

### 5.3.6 Mapendekezo

Utafiti huu ulitoa kumbukumbu za marejeleo ambazo wasomi watatumia ili kufanya tafiti nyingine miongoni mwa jamii mbalimbali na kutoa mwelekeo ambao serikali kuu na Kaunti zaweza kutumia ilikuleta suluhu miongoni mwa jamii wakati wa mitafaruku na vita. Migogoro, mizozo na ugomvi ni hali ya kawaida miongoni mwa wanajamii na watu wenye mahusiano mbalimbali. Kila kundi la watu lina mipango yao wenyewe ya kukabiliana na migogoro na kutatua mizozo kati ya wanajamii kulingana na (Ajayi & Buhari, 2014). Wanaongezea kuwa jamii mbalimbali za Afrikana hata Kenya wana njia anuwai za kusuluhisha mizozo kati ya wanajamii wao. Utafiti huu utafaidi katika kuleta suluhu, amani na utengamano miongoni mwa

jamii mbali mbali Kenya na kote ulimwenguni. Utafiti huu utasaidia katika uelewa wa ulimwengu wa jamii mbalimbali kupitia uchanganuzi wa lugha ya urejelezi wanayoitumia jamii zinazopakana katika suala la lugha ya urejelezi na athari zake. Mazungumzo yao ni amali kuu katika kuelewa ufasiri wao wa ujinsia na kupata uangavu wa sababu za mwelekeo wa maamuzi na matendo yao. Kwa hili, mtafiti anapendekeza yafuatayo:

i) Wanaobuni sera hawana budi kushirikisha lugha ya urejelezi katika uundaji wa sera zao ilikusuluhisha mitafaruku inayotokana na matumizi ya urejelezi miongoni mwa jamii zinazopakana.

ii) Iwapo jamii pana itataka kujua, kuelewa na kutatua tatizo la kutoelewana miongoni mwa jamii kuna ithibati kuwa urejelezi huzua kutoelewana na hatimaye vita kati ya jamii.

iii) Suala zima la urejelezi ni hali ya kuzingatiwa na viongozi na jamii kwa jumla.

